
Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 20 | Januari 15, 2022 NAKALA BILA MALIPO




# JUBILEE ILIVYOTEKA MRADI WA SH160B

**Mradi huo wa mabilioni ya pesa wa Barabara Kuu ya Rironi-Nakuru-Mau Summit ulipewa kampuni fulani ikisaidiwa na afisa wa Ikulu mwenye nguvu, licha ya makosa kugunduliwa na Wizara ya Fedha. Tunafichua mivutano kuhusu mradi huo na maswali magumu yanayoulizwa na utawala wa Ruto**

# The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore

## anywhere, anytime.

Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**8 KIZUIZI CHA MRADI WA BARABARA KUU YA MAU SUMMIT:** Kufifia kwa mradi huo kunahusishwa na kutoweka kwa ushawishi wa wasaidizi wa kisiasa wa kampuni ya Ufaransa iliyopewa kandarasi ya ujenzi wa mradi huo mkubwa.

**10 MCHAPA KAZI MTEULE WA RAIS:** William Ruto anatafuta mtu asiye mbishi kutekeleza ajenda yake ya kiuchumi ikizingatiwa kwamba kuna upinzani wenye nguvu na inaonekana mtu huyo ni Musalia Mudavadi.

**16 KICHEKO KWA WINGI:** Video za ucheshi kuhusu maisha ya kawaida za muundaji matini Muchiri Mike katika TikTok zimemfanya maarufu sana na zinamletea pesa.

**27 MASAIBU YA MWANAMFALME:** Kitabu kipya cha Prince Harry kinasimulia kwa upana visa vinavyojulikana lakini mambo machache mapya.




# Mzozo wa ujenzi wa Barabara Kuu ya Nakuru lazima usuluhishwe kisheria



Washington Gikunju

**Usafiri kwa Pasaka, Krismasi na sikukuu nyingine za kitaifa umekuwa wa kubahatisha, wasafiri huwa hawajui iwapo watafika kwa wakati kuungana na wapendwa wao mashambani au sehemu wanakoenda likizo. Ndiyo sababu habari kwamba sehemu hiyo ya kilomita 233 ya barabara hiyo kuu kati ya Nairobi na Mau Summit ingepanuliwa zilipokewa kwa matumaini makubwa.**

Kuendesha gari katika Barabara Kuu ya Nakuru ni kazi ngumu na kunachosha akili na kumejaa hatari ya magari kugongana huku madereva wakijaribu kupita malori yanayoendeshwa kwa mwendo wa konokono.

Magari karibu 20,000 yanakadiriwa kupitia barabara hii kuu inayojaa msongamano kila siku, baadhi yakiwa yameanza safari yake kutoka zaidi ya kilomita 1000 katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Baadhi ya wasafiri huwa hawafiki yanakoenda kwa kuwa ajali nyingi huwaacha wamekufa au kujeruhiwa.

Barabara hiyo hupatia nchi habari za baadhi ya ajali mbaya zaidi huku baadhi ya sehemu zikiwa zimewekwa alama kuonyesha ni hatari sana.

Juhudi za kuunda upya na kupanua baadhi ya sehemu hatari hazijazaa matunda, kwa kuwa magari katika barabara hiyo yanaongezeka kwa kiwango kinachokadiriwa kuwa asilimia nne kila mwaka. Isipokuwa kwenye habari kwa sababu ya ajali, Barabara kuu ya Nakuru hugonga vichwa vya habari kwa sababu ya misongamano ya urefu wa kilomita kadhaa.

Kutatizika kidogo kwa safari za magari katika kituo cha kupima uzani cha Gilgil kunafanya maelfu ya Wakenya kulala kwenye baridi ya usiku katika msongamo wa magari kwa sababu ya ukosefu wa nafasi ya kuwezesha magari kukwepa mkwamo huo.

Usafiri wakati wa Pasaka, Krisimasi na sikukuu nyingine za kitaifa umekuwa wa kubahatisha, wasafiri huwa hawajui kama watafika wanakoenda kwa wakati kujumuika na wapendwa wao mashambani au sehemu za likizo. Hii ndiyo sababu habari kwamba sehemu ya kilomita 233 ya barabara hiyo kati ya Nairobi na Mau Summit ingebadilishwa kuwa ya pande mbili zilipokewa kwa furaha na matumaini makubwa. Haikujalisha iwapo pendekezo lilikuwa la kufanya barabara hiyo kuwa ya kulipiwa, madereva ambao wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu walikuwa tayari kulipa ili kuepuka tatizo hilo la kila mara.

Kile ambacho Wakenya wengi hawakufahamu, hata hivyo, ni kwamba kutolewa kwa kandarasi ya Sh160 bilioni kwa kampuni ya Ufaransa, Vinci, kulijaa dosari. Kama habari kuu katika toleo la wiki hii inavyofichua, makosa katika kuhesabu ushuru yalipuuzwa wakati wa mchakato wa kutoa zabuni. Hii ndiyo sababu mwanakandarasi kutoka Ufaransa alimshinda mshindani wake wa Ureno Mota Engil Group, licha ya malalamishi ya Wizara ya Fedha.

Sasa nguvu za siasa zimebadilika, na makosa yaliyotajwa kuwa madogo katika ushindi wa kandarasi ya Vinci, yanasumbua kampuni hiyo ya Ufaransa. Bila shaka kuna kuna siasa zinazoendelea kisiri, ambazo zitaamua ni kampuni ngani itafaulu, au iwapo kandarasi hiyo itafutiliwa mbali.

Hayo yakiendelea, maelfu ya madereva wanaendelea kuteseka kwa kukwama kwa saa nyingi katika barabara kuu hiyo kila siku. Uchumi unaendelea kupoteza mabilioni ya pesa kupitia mafuta yanayoharibika, saa za kazi kupotezwa na maeneo maarufu ya watalii kukosa wateja, makosa yake yakiwa kuwa katika au baada ya barabara hiyo yenye msongamano.

Gharama ya kupanua barabara hiyo pia inaendelea kuongezeka, kulingana na kiwango cha mfumuko. Hali haikufaa kuwa hivi. Kulikuwa na fursa ya kufanya kilichokuwa sahihi na kutoa zabuni hiyo ipasavyo tangu mwanzo. Tenda inayotolewa kwa kufuata utaratibu huwa stakabadhi isiyoweza kukiukwa, hata baada ya mabadiliko ya afisi za kisiasa.

Pia, inafanya walipa ushuru kuokoa muda mwingi na pesa nyingi. Hatua zozote ambazo serikali ya Kenya Kwanza itachukua kuendelea mbele kuhusiana na kandarasi hii ni lazima izingatie sheria.

*wgikunju@ke.nationmedia.com*

*-Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki

Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno

**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri

**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji

**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Chebukati, Guliye na Molu wafunga virago

# Makamishna wa IEBC watoka afisini


Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) Wafula Chebukati na makamishna Profesa Abdi Guliye na Boya Molu wataondoka afisini wiki hii baada ya kumalizika kwa muhula wao wa miaka sita.

Watatu hao waliteuliwa mnamo Januari 18, 2017 na aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta. Kuondoka kwao kutafuatia mchakato wa kuteua makamishna wapya na mwenyekiti.

Kamishna Irene Masit anachunguzwa na jopokazi linaloongozwa na Jaji Aggrey Muchelule. Makamishna wanne wakiongozwa na Juliana Cherera walisimamishwa kazi mwaka uliopita baada ya kupinga matokeo ya urais yaliyotangazwa na Chebukati.

Wengine ni Justus Nyang'aya na Francis Wanderi. Macho yote sasa yameelekezwa kwa nani atakayeunda jopokazi la uteuzi la IEBC baada ya Rais William Ruto kuchapisha notisi kwa umma mwaka uliopita kubuni jopokazi hilo.

Sheria ya IEBC inamhitaji Rais kuteua jopokazi la uteuzi la wanachama saba angalau miezi sita kabla ya kukamilika kwa muhula wa mwenyekiti au kamishna ili kuanza mchakato wa uteuzi.



Mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati (katika) akiwa na makamishna Profesa Yusuf Guliye (kushoto) na Molu Boya katika jumba la Anniversary Towers Aprili 20, 2018.

■ 'Wananuia kushindana karibuni iwezekanavyo'



Max Verstappen wa kampuni ya Red Bull wakati wa mashindano ya Grand Prix jijini Suzuka, jimbo la Mie, Japan, Oktoba 9, 2022.

# Andretti yaungana na GM kuingia F1

Timu ya Amerika ya Andretti Global imeungana na shirika maarufu la kuunda magari Amerika General Motors ikinuia kuingia mashindano ya Formula 1.

Taarifa ya pamoja ilisema GM itawakilishwa na gari lake la kifahari aina ya Cadillac. Mwenyekiti wa Andretti Global Michael Andretti alisema: "Tunafaa kabisa kuwa timu mpya ya F1 na tunaweza kuleta thamani kwenye mashindano hayo."


Andretti alisema "anajitahidi kushindana karibuni iwezekanavyo." Alisema anataka "angalau dereva mmoja wa Amerika."

Mgombeaji mkuu wa nafasi hiyo ni dereva wa IndyCar Colton Herta, ambaye hushiriki mashindano hayo kwa Andretti, ana maazimio ya F1 na alikosa wadhifa huo mwaka huu na timu ya Red Bull ya Alpha Tauri kwa sababu tu hakuwa na pointi za kutosha.

Mwenyekiti wa Cadillac Mark Reuss alisema: "Tuna historia ndefu ya mashindano ya mbio za magari na tuna furaha kuhusu uwezekano wa kushirikiana na Andretti Global kuunda timu ya F1 ya Amerika itakayosaidia kuchochea mvuto hata zaidi kimataifa katika mashindano hayo ."Cadillac na F1 zote zina umaarufu unaozidi kupanda duniani. Nembo yetu ina sifa ya mashindano ya mbio za magari ambayo imekuwa ikiundwa kwa zaidi ya karne moja, na tutajivunia kuwa na fursa ya kuleta ubunifu na muundo wetu wa kipekee wa Amerika katika F1."

■ Kagame: Huu kamwe si mzigo wetu

# Rwanda yakataa wakimbizi wa DRC



Rais wa Rwanda Paul Kagame amesema nchi yake haitawapa tena hifadhi watu wanaotoroka vita Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Mapigano ya miaka mingi eneo la mashariki yamelazimisha wakimbizi wengi kuvuka mpaka kuingia Rwanda. "Hili si tatizo la Rwanda," akasema Kagame na kuongeza: "Nimekataa kuwa Rwanda inafaa kubeba mzigo huu." Alisema mataifa mengine ya dunia hayaelewi masuala kuhusu mashariki mwa DRC. Tishio halisi la usalama – kwa maoni yake – ni kile anachotaja kuwa mabaki ya vikosi vya waasi wa Kihutu waliojaribu kuangamiza kabila lake la Watutsi katika mauaji ya halaiki ya 1994

■ Hasira kuhusu video iliyonaswa ikulu ya rais

# Video: Rapa aomba Ghana msamaha



Mwanamuziki wa rapa raia wa Amerika Meek Mill ameomba radhi baada ya kuibua hasira nchini Ghana kwa video ya muziki iliyonaswa katika ikulu ya rais.

Vyombo vya habari viliripoti kuwa watu walikasirishwa na walichohisi kuwa "kuchafuliwa" kwa urais na Meek Mill na masuala ya usalama kwa kunasa video ya muziki katika jumba la hadhi ya juu kiasi hicho. Video hiyo kwanza iliwekwa katika akaunti ya Instagram ya Meek Mill Jumapili iliyopita.


Mnamo Jumatatu, rapa huyo aliwaomba radhi raia wa Ghana na afisi ya rais kupitia Twitter. Alisema: "Naomba watu msamaha kama niliwakosea heshima kwa namna yoyote. . .naomba radhi kwa afisi pia."

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

Nation Media Group©

kurunzi ya kenya

■ 'WATU KARIBU 10 WALIIBA MABILIONI KUPITIA USHAWISHI WA KIBIASHARA'




# UTEKAJI SERIKALI: UKWELI MCHUNGU

## Ingawa Ruto ni mwangalifu na mkweli kuhusu suala la uchunguzi wa mahakama, wengi wanaomzunguka wanataka amkabe kabisa Uhuru, himaya ya biashara za iliyokuwa Familia ya Rais na maafisa wakuu katika

• Na MACHARIA GAITHO

Mwanasheria Mkuu Justin Muturi anatoa mfano wa Amerika na Brazil kusisitiza ni kwa nini ni muhimu ukweli usemwe kuhusu dai la 'mapinduzi' kabla ya William Ruto kutangazwa mshindi wa uchaguzi wa urais 2022.

Hii ni kufuatia madai kuwa maafisa wakuu wa serikali mnamo Agosti 15, katika Kituo cha Kitaifa cha Kujumlisha Matokeo cha Bomas of Kenya, walijaribu kumsukuma Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka Wafula Chebukati 'kukarabati' matokeo ili Raila Odinga atangazwe mshindi, au atoe nafasi ya raundi ya pili ya uchaguzi dhidi ya Ruto.

Rais Ruto ametaja dai hilo la kumpokonya ushindi kuwa mojawapo la masuala muhimu ya tume itakayoundwa kuchunguza 'Utekaji wa Serikali' chini ya mtangulizi wake Uhuru Kenyatta. Watu mashuhuri katika serikali ya Kenya Kwanza, akiwemo Naibu Rais Rigathi Gachagua, wanasisitiza uhalifu unaodaiwa kutekelezwa na utawala wa Uhuru uchunguzwe.

Ruto mwenyewe aliahidi uchunguzi kuhusu Utekaji wa Serikali katika kampeni zake, na mnamo Januari 4 akihojiwa na vituo kadhaa vya televisheni, aliorodhesha makosa aliyodai yalifanywa na serikali aliyohudumu kama Naibu Rais kwa miaka kumi. Yalijumuisha njama ya kubadilisha matokeo ya uchaguzi, ambayo ilihusisha jeshi; mauaji ya kiholela yaliyotekelezwa na polisi, kukamatwa na kushtakiwa kwa wafuasi wake; kuondolea ushuru biashara za kibinafsi; Reli ya Kisasa na kandarasi zingine kubwa za miundomsingi; na kutengea watu binafsi ardhi ya serikali ikiwemo sehemu ya mradi wa unyunyizaji uliokwama wa Galana Kulalu.

Hata hivyo, Rais alionya kuwa huenda uchunguzi kamili hautafany hivi sasa kwa sababu lazima achunge maslahi mengine. "Nitarekebisha uchumi au nitashughulikia kitu

Endelea Uk 6

Nation Media Group ©

kurunzi ya kenya

# Makosa ya awali: Ruto ashikilia kiazi moto

Kutoka Uk 5

hiki kikubwa ambacho kitafyoza nguvu zetu?" akauliza. Kulingana na Muturi, serikali inawazia Tume ya Mahakama kama iliyoundwa na Rais Kibaki 2003 kuchunguza kashfa ya Goldenberg, lakini pia itatafuta njia zingine.

Fujo alizochochea aliyekuwa Rais wa Amerika Donald Trump baada ya kukataa kushindwa katika uchaguzi na kusababisha uvamizi wa majengo ya Bunge ya Amerika na umati uliozua ghasia Januari 6, 2021, na mashambulizi sawa ya hivi majuzi nchini Brazil, ambako wafuasi wa Rais aliyeshindwa Jair Bolsonara Jumapili iliyopita walivunja na kuingia katika Bunge, Mahakama ya Upeo na Ikulu ya Rais, yanaeleza hatari ya walio mamlakani kukataa kushindwa katika uchaguzi.

Ingawa Rais Uhuru Kenyatta hakuwa mgombeaji katika uchaguzi mkuu wa Agosti iliyopita, aliunga mkono hadharani mgombeaji wa upinzani Odinga dhidi ya Ruto ambaye wakati huo alikuwa Naibu Rais. Ndiye aliyekuwa na nguvu za kutuma maafisa wakuu wa serikali Bomas of Kenya katika juhudi ambazo hazikufaulu za kubadilisha au kudanganya katika uchaguzi, na kwa hivyo, atakuwa mtu muhimu kizimbani uchunguzi ukifanywa.

Kulingana na Muturi, hata hivyo, uchunguzi kama huo, ambao utaonekana kumlenga mtangulizi wa Ruto, ni lazima ufanywe kwa tahadhari kubwa ikizingatiwa kuwa demokrasia ya Kenya ni tete. Mwanasheria Mkuu alikiri katika gumzo na Darubini ya Wiki kuwa hakuna mwongozo wa wazi kuhusu jinsi uchunguzi kama huo utakuwa, akikubaliana na Rais kuwa hakuna haja ya kuharakisha kufanya jambo linaloweza kuchukuliwa kuwa kisasi cha kisiasa na linaloweza kugawanya taifa.

Kwa hivyo, haja ya kufichua maovu ya serikali ya Uhuru na kuadhibu waliohusika na utumiaji mbaya wa mamlaka, ufisadi na makosa mengine ni lazima ipimwe dhidi ya maslahi mapana ya kitaifa na pia isiondoe umakinifu kutoka ajenda ya maendeleo ya Serikali ya Kenya Kwanza.

Ingawa Ruto ni mwangalifu na mkweli kuhusu suala la uchunguzi, kuna wengi wanaomzunguka, hasa wanasiasa vijana, wanaharakati wa chama na maafisa wapya serikalini wanaotaka kupuuza tahadhari na kumuandama Uhuru, biashara za iliyokuwa Familia ya Rais na maafisa wakuu wa serikali iliyopita. Gachagua amekuwa miongoni wanaotaka utawala wa Uhuru uchunguzwe, akisisitiza katika mahojiano na Televisheni ya Inooro Jumapili iliyopita kuwa uchunguzi kuhusu Utekaji wa Serikali utapelekea kutwaliwa kwa utajiri unaodaiwa kupatikana na watu muhimu katika serikali iliyoondoka.

Hata hivyo, Naibu Rais, shingo upande, hakusisitiza kuanzishwa kwa mfumo rasmi wa uchunguzi kama Tume ya Mahakama au Tume ya Rais kwa sababu muhimu zaidi ni ajenda ya serikali ya kupunguza gharama ya maisha. Hivyo basi haileweki wazi jinsi waliohusika na maovu watatambuliwa na kuadhibiwa bila kuwepo kwa mfumo rasmi wa uchunguzi. Alisema mtandao wa ufisadi unaodaiwa ulijumuisha "watu wapatao 10 waliopora mabilioni kutoka kwa uchumi kupitia ushawishi wa kibiashara".

Katika kinachoweza kumaanisha biashara za familia ya Kenyatta, alidai mitandao hiyo inamiliki benki na kudhibiti viwango vya riba, na kuwa kila sera ya umma iliundwa ili kuipatia faida kubwa. Alidai familia zenye ushawishi zilihusika na mitandao inayotawala sekta za maziwa, chai na kahawa na ilikuwa ikipinga mageuzi ili iendelee kufanya wakulima watumwa, akisema hata ilikopa pesa kulipa bonasi kutoka kwa benki 'Mkubwa'. "Hatutalipa mikopo hiyo kwa kuwa haikuidhinishwa na wakulima," akasema.

"Hakika tutafuta hatimiliki za mashamba yao walizopata kwa njia haramu, mikataba na biashara," alitamatisha, lakini hakutaja kuwa hilo litakuwa kupitia mchakato rasmi wa agizo la serikali. Alilaumu mitandao hiyo, ambayo pia hakufichua, kwa kuhusika na ufisadi katika polisi na mauaji ya kiholela. "Maafisa wote na wakubwa wao walioua Wakenya… na kufanya watu mayatima na wajane…huenda tusiwaandame lakini hamtawahi kupata amani," akasema, pia bila kutaja jinsi wahusika watatambuliwa. Pia, hakueleza jinsi wataadhibiwa bila uchunguzi rasmi, kushtakiwa na kupatikana na hatia.


Alifichua kuwa mkutano wa kikazi wa siku nne wa serikali katika Fairmont Mt Kenya Safari Club uliamua kuacha uchunguzi wa Utekaji wa Serikali ili serikali iweze kuzingatia kutimizia Wakenya ahadi, akizua maswali tena kuhusu jinsi ahadi ya kuwaadhibu waliohusika na visa mbalimbali vya uhalifu itatimizwa.

Kwa sasa, hata hivyo, tishio la uchunguzi kuhusu Utekaji wa Serikali linaweza kuwatia hofu maafisa wengi wa serikali iliyopita. Anayefaa kuwa na hofu zaidi ni Rais mstaafu, ambaye bila shaka atakuwa wa kwanza kizimbani iwapo uchunguzi utafanywa kuhusu jaribio la kubadilisha matokeo ya uchaguzi wa urais.

Kulingana na maelezo ya Chebukati kuhusu tukio hilo katika Bomas of Kenya, ujumbe wa Kamati ya Ushauri Kuhusu Usalama wa Kitaifa uliojumuisha Katibu Msimamizi katika Afisi ya Rais Kennedy Kihara, Wakili Mkuu wa Serikali Kennedy Ogeto, Inspekta Jenerali wa Polisi Hillary Mutyambai na Makamu Mkuu wa Majeshi Luteni Jenerali Francis Omondi Ogolla, ulijaribu kumwekea presha abadilishe matokeo na kuacha kumtangaza Ruto kuwa mshindi. Alidai Mkuu wa Utumishi wa Umma Joseph Kinyua alikuwa amempigia simu na kumuomba apokee timu hiyo.

Maelezo ya Chebukati katika taarifa kwa vyombo vya habari na hati ya kiapo aliyowasilisha kujibu kesi ya Raila katika Mahakama ya Upeo kupinga ushindi wa Ruto, yaliongezea hali ya kutia hofu katika mzozo huo wa uchaguzi. Yalipingwa na Kihara na Kinyua wakiyataja kuwa madai ya kuchochea na kuharibu sifa za taasisi muhimu za serikali kwa kuzipaka tope. Hata hivyo, Ruto anatumia maelezo hayo kuthibisha tukio ambalo lingekuwa sawa na mapinduzi dhidi ya mgombeaji aliyechaguliwa kihalali na utumiaji wa jeshi ambao haujawahi kushuhudiwa.

Kuhusu matukio katika Bomas of Kenya, wengi waliohusika tayari wameondoka seri-



Rais William Ruto

Nation Media Group©

kurunzi ya kenya

kalini au mamlaka yao kupunguzwa baada ya utawala mpya kuingia mamlakani. Hata hivyo, uchunguzi unaweza kuathiri kazi za baadhi yao, kama vile Luteni Jenerali Ogolla, ambaye kwa utaratibu wa kawaida angekuwa mrithi wa Jenerali Robert Kibochi kama Mkuu wa Majeshi baadaye mwaka huu. Kama kulikuwa na jaribio kama hilo inavyodaiwa, kuna uwezekano mkubwa kuwa ujumbe huo haungetembelea Chebukati kwa shughuli kama hiyo bila maagizo ya Rais mstaafu, au ufahamu wake na idhini yake. Ni wazi kuwa Uhuru ndiye atakuwa akilengwa.

Uchunguzi kuhusu suala hilo pia untamhusisha aliyekuwa Waziri wa Usalama wa Ndani na Ushirikishi wa Serikali ya Kitaifa Fred Matiang'i, ambaye katika muhula wa mwisho wa urais wa Uhuru alitwikwa nguvu ambazo zilionekana kuzidi za Ruto. "Waziri Mwenye Nguvu" alivyojulikana, hakusimamia idara zenye nguvu za usalama na utawala pekee, lakini pia alikuwa kama waziri mkuu katika yote aliyofanya isipokuwa jina kwa kuwa alisimamia kamati za mawaziri ambazo mawaziri wenzake wote waliripoti. Alichukiwa na washirika wa Ruto, ambao walimuona kuwa aliyetwaa nguvu za Naibu Rais. Pia walimwekelea madai mengi kuhusu ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka, baadhi ambayo walio katika serikali mpya wangetaka kuendeleza.

Katika wizara ya usalama wa ndani ya serikali iliyoondoka, mtu mwingine ambaye washirika wa Ruto wangependa kuona ameadhibiwa pamoja na Matiang'i ni aliyekuwa Katibu wa Usalama wa Ndani Karanja Kibicho. Katika muhula wote wa mwisho wa serikali ya Jubilee, mtandao wa propaganda wa Ruto katika mitandao ya kijamii, ukiongozwa na mwanamikakati wa dijitali Dennis Itumbi, uliendesha mashambulizi dhidi ya wawili hao, ukiwalaumu kwa kila aina ya uhalifu na maovu. Timu hiyo ilihusika kuzua madai ambayo hawakuthibitisha ya mkutano wa Mada Hotel kuhusu njama ya kumuua Naibu Rais, na pia madai kuhusu kashfa ya ardhi ya Ruaraka.

Mnamo Desemba 2021, Itumbi alipotekwa nyara na kupigwa vibaya na watu wasiojulikana, akalazwa wiki kadhaa hospitalini akiwa amevunjika miguu na mikono, alilaumu maafisa wa usalama kwa shambulizi hilo. Maoni yake yaliungwa mkono na Ruto kuonyesha wazi sababu ya kuzidi kuwashambulia Matiang'i na Kibicho, na pia Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai George Kinoti.

Pengine Itumbi atataka sana kulipiza kisasi kwa wale anaodai walimtesa. Lakini uchunguzi kuhusu shambulizi la Desemba 2021 pia utafufua kisa kingine cha miezi michache iliyotangulia mtu alipompigia simu kudai gari lake lilikuwa likifuatwa na kufyatuliwa risasi na watu wasiojulikana. Aliripoti katika Kituo cha Polisi cha Kasarani kuhusu alichodai lilikuwa jaribio la kumuua, lakini wnaojua kisa hicho, wakiwemo washirika wake wa karibu, walitilia shaka madai hayo, wakishuku tukio hilo lilipangwa kama sehemu ya kuzuia polisi ambao walikuwa wakimsaka.

Kinoti, ambaye aliondoka ofisini punde tu Ruto alipoingia mamlakani, ni mwingine aliye na sababu ya kuwa na wasiwasi. Rais alifichua katika mahojiano na televisheni kuwa alimfuta kazi mkuu huyo wa DCI, kinyume na maelezo yake alipoingia ofisini kuwa alikuwa amekubali kujiuzulu kwake. Darubini ya Wiki ilipowasiliana na Kinoti alikataa kuzungumza zaidi isipokuwa tu kuthibitisha kuwa anaendelea vyema.

Hata hivyo, anajua anaweza kuandamwa kutokana na jinsi washirika wa Ruto walimlaumu vikali kwa kuwalenga kwa msururu wa uchunguzi na mashtaka yaliyotegemea ushahidi wa uongo.

Nyingi za kesi za ufisadi na uhalifu ambazo Kinoti alisukuma – zikiwemo dhidi ya Gachagua na Mawaziri Aisha Jumwa na Mithika Linturi – ziliondolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma Noordin Haji punde tu Ruto alipoingia mamlakani. Hatari zaidi ni kuwa Kinoti sasa analaumiwa kwa visa vya mauaji ya kiholela, huku Ruto akidai kontena ya mizigo katika kituo cha polisi Nairobi ilitumiwa kama eneo la kutesa na kuua watu.

Punde tu serikali mpya ilipoingia mamlakani, ilishinikiza uchunguzi kuhusu utekaji nyara na kushukiwa kuuawa kwa wataalamu wawili wa IT raia wa India mnamo Julai mwaka jana ambao walikuwa wameajiriwa na kampeni ya Ruto, Mohammed Said Samina na Zulfiqar Ahmad Khan na dereva wao wa teksi, Nicodemus Mwania. Maafisa wanane kutoka kikosi cha DCI kilichovunjwa waliolaumiwa kwa mauaji hayo walikamatwa lakini mlengwa mkuu anaweza kuwa alikuwa na wajibu wa mamlaka. Mbali na operesheni za usalama, uchunguzi kuhusu Utekaji wa Serikali unaweza kuhusisha madai ya utumiaji mbaya wa mamlaka kunufaisha biashara za kibinafsi.

Ruto na Gachagua wamekuwa wakitaja kuunganishwa kwa Benki ya Kibiashara ya familia ya Kenyatta ya Commercial Bank of Africa na NIC Bank kuunda NCBA Bank kuwa zilizonufaika kutokana na kuondolewa ushuru wa zaidi ya Sh300 milioni hatua iliyomfanya aliyekuwa Waziri wa Fedha Ukur Yattani kulaumiwa.

Gachagua, ambaye amepewa jukumu la kusimamia mageuzi ya sekta ya kilimo, tangu wakati wa kampeni amekuwa akilaumu familia ya Kenyatta kwa kutawala biashara ya maziwa kupitia kampuni yao ya Brookside ambayo imenunua kampuni zote kubwa zilizokuwa washindani wake.

Ingawa hajawahi kutoa ushahidi wowote, amekuwa akidai kuwa mitandao inayohusishwa na iliyokuwa Familia ya Rais imetumia ushawishi wa kisiasa kujikita katika sekta tofauti za kilimo, ikiwemo maziwa, kahawa na chai. Ahadi yake ya kutwaa mali iliyopatikana kwa ufisadi inaweza kuzua hofu katika sekta tofauti lakini pia anaweza kukanyaga eneo telezi iwapo hatua kama hizo hazitatokana na mchakato wa mahakama kuliko matamshi katika mikutano ya kisiasa.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



Mwanasheria Mkuu Justin Muturi

kurunzi ya kenya

■ MAAFISA WAKUU WAMEZUA MASWALI KUHUSU MANUFAA YA MRADI HUO



**SH 160 BILIONI**

Mradi wa barabara kuu ya kulipia ya Nairobi-Nakuru-Mau Summit ndio mkubwa zaidi Afrika, ukiungwa mkono na serikali ya Ufaransa na taasisi kadhaa za maendeleo za kimataifa zenye ushawishi

Vinci Group ilitoza Sh5.3 bilioni kila miezi mitatu huku Mota Engil ikitoza Sh6.2 bilioni, kumaanisha kuwa – kwa mtazamo wa haraka- kampuni ya Ufaransa ndiyo ilitoza ada nafuu

Mradi huo utajumuisha upanuzi wa barabara hiyo, ujenzi wa barabara ya kilomita nne kupitia juu ya Mji wa Nakuru and ujenzi wa sehemu nyingi za kuingilia na kutokea

Uamuzi wa serikali ya Rais Ruto wa kusimamisha mradi huo utaathiri vibaya uhusiano wa kidiplomasia na serikali ya Ufaransa

**2018**

Mradi huo ambao ulichorwa na Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu Kenya (KeNHA) mnamo 2018 na kupewa kundi la kampuni la EPC la Ufaransa,, Vinci Group, ulijadiliwa chini ya mpango wa ushirikiano wa sekta ya kibinafsi na ya umma

**MAGARI 20,000 KWA SIKU**

Takwimu za KeNHA zinaonyesha kuwa barabara hiyo inatumiwa na magari yanayokadiriwa kuwa 20,000 kwa siku na idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kwa asilimia nne kila mwaka

# MZOZO KUHUSU UJENZI WA BARABARA KUU YA NAKURU

## Kufifia kwa mradi huo kunahusishwa na kukosa ushawishi kwa wanasiasa wanaounga mkono kampuni ya Ufaransa iliyopewa kandarasi hiyo kubwa baada ya kushindana na kampuni kubwa ya ujenzi ya Ureno

• Na JAINDI KISERO

Je, serikali mpya ya Rais William Ruto inataka kusimamisha mradi wa ujenzi wa barabara ya Nairobi-Nakuru-Mau Summit wa gharama ya Sh160 bilioni - mradi mkubwa wa ushirikiano wa sekta ya umma na serikali Afrika unaoungwa mkono na serikali ya Ufaransa na taasisi zingine za maendeleo ya kimataifa zenye nguvu?

Sakata hiyo imeibua funzo kuu kuhusu masaibu ya miradi mikubwa ya miundomsingi, yanayoweza kukumba utekelezaji wake ukihusisha tawala kadhaa serikali mpya inapoingia mamlakani.

Ripoti za vyombo vya habari wiki hii zilifichua kuwa serikali mpya imeamua kusimamisha unaochukuliwa kuwa mradi ghali zaidi wa barabara wa Rais mstaafu Uhuru Kenyatta.

Mradi huo ambao ulichorwa na Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu Kenya (KeNHA) mnamo 2018 na kupewa kundi la kampuni la EPC la Ufaransa,, Vinci Group, ulijadiliwa chini ya mpango wa ushirikiano wa sekta ya kibinafsi na ya umma (PPP), kumaanisha kuwa kampuni hiyo ya Ufaransa inajenga barabara hiyo, kuimiliki na kuisimamia kwa miaka 30 huku serikali ikikusanya ada kutoka kwa watumiaji wa barabara hiyo. Sharti muhimu katika makubaliano hayo ni kuwa, ni lazima serikali ianzishe hazina ya taifa ya ada ambapo pesa za kulipa mwanakandarasi zitatoka.

Ikiwa hatua kubwa zaidi ya Kenya kukabiliana na msongamano usioisha katika eneo muhimu la Uchukuzi la Kaskazini, umuhimu

Nation Media Group ©

## kurunzi ya kenya

wa kiuchumi wa mradi huo hauwezi kupuuzwa. Takwimu za KeNHA zinaonyesha barabara hiyo inatumiwa na magari yanayokadiriwa kuwa 20,000 kwa siku na idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kwa asilimia nne kila mwaka. Kazi ya mradi huo itajumuisha kupanua barabara hiyo, kujenga barabara ya juu ya kilomita nne kupitia mji wa Nakuru na mizunguko kadhaa kwenye barabara hiyo ya kilomita 233.

Kufikia sasa, mradi huo, utakaofadhiliwa kwa pesa kutoka sehemu tofauti, ikiwemo Vinci Group, mapato ya kwanza kutoka sehemu zitakazokamilika, deni kubwa kutoka mashirika ya kimataifa ya ufadhili chini ya Benki ya Dunia, mikopo ya biashara iliyodhaminiwa na mashirika ya Amerika na mikopo ya humu nchini bado haujapata pesa.

Uamuzi wa serikali ya Rais Ruto wa kusimamisha mradi huo utakuwa na athari kwa uhusiano wa kibalozi na serikali ya Ufaransa, ambayo inauunga mkono, ikiuchukulia kuwa nafasi nzuri kwa wanakandarasi wake kushiriki katika kazi ambayo imetawaliwa na wanakandarasi wa China. Ukisimamishwa, pia kutakuwa na athari kwa uhusiano na taasisi za kifedha za maendeleo ya kimataifa zinazounga mkono mradi huo.

Sakata hiyo pia imechochewa na siasa. Wachanganuzi wanahusisha kufifia kwa mradi huo na kukosa ushawishi wa kisiasa wa wanaounga mkono kampuni ya Ufaransa iliyopewa kandarasi hiyo kubwa baada ya ushindani mkali na kampuni kubwa ya ujenzi ya Ureno, Mota Engil Group. Ingawa jambo hili halizungumziwi hadharani, ukweli wa siasa za miradi mikubwa ya miundomsingi Kenya mara nyingi hulazimisha wawekezaji wa kimataifa kuwa na ushirikiano wa kisiasa - mawakala wa humu nchini wenye ushawishi na jamaa za wakuu katika Ikulu kusaidia wageni hao kushinda changamoto za kutimiza maslahi yao. Kubadilika kwa uongozi katika Ikulu kunaweza hata kubadilisha hali ya mradi mzuri.

Katika kisa cha Barabara Kuu ya Nairobi-Mau Summit, kuhusika kisiasa chini kwa chini katika ununuzi kulikuwa na nguvu hivi kwamba mchakato wa utathmini ulikumbwa na utata na madai ya kuingiliwa na mawakala waliokuwa na ushawishi wa kisiasa. Kampuni ya Ufaransa ilisemekana kuungwa mkono na ajenti wa kujitegemea aliye na uhusiano wa karibu na Ikulu ya Rais mstaafu Uhuru Kenyatta, huku mawakala wa Mota Engil Group na mwanasiasa aliyeiunga mkono akiwa mwanawe waziri wa zamani katika serikali ya Mwai Kibaki.

Mawasiliano yaliyoonekana na Darubini ya Wiki yanaonyesha ni Kitengo cha PPP cha Wizara ya Fedha – shirika linalohakikisha kuna uwazi na uwajibikaji katika miradi yote ya PPP - kilichofichua njia isiyokuwa ya kisheria ambayo tenda hiyo ilitolewa kwa Vinci Group.

Stakabadhi zinaonyesha kuwa wakati wa awamu za utathmini wa kina wa kifedha, iligunduliwa kuwa kundi hilo la Ufaransa lilikuwa limefanya kosa kubwa katika kuhesabu ushuru wa mapato katika zabuni yake.

Pia iliibuka kuwa KeNHA iliamua kufumbia macho kosa hilo lililotambuliwa na Kitengo cha PPP katika zabuni ya kampuni hiyo ya Ufaransa kwa misingi kuwa makosa hayo yalikuwa madogo, ikitumia sehemu katika stakabadhi za zabuni zilizoruhusu upande unaotoa kandarasi kupuuza na kutupilia mbali masuala madogo. Mawasiliano hayo pia yanaonyesha kuwa baada ya kuamua kupuuza makosa hayo, KeNHA ilisonga mbele na kuuliza Vinci kuyarekebisha. Stakabadhi hizo zilipowasilishwa kwa Kamati ya Uchunguzi ya PPP, kamati hiyo iligundua makosa hayo katika zabuni ya Vinci. Katika barua kwa KeNHA iliyoandikwa Novemba 13, 2018, Katibu wa Wizara ya Fedha Dkt Kamau Thugge alisema kamati yake ilikuwa imefikia uamuzi kuwa makosa katika zabuni ya Vinci hayakuwa madogo.

Bila kutatuliwa, alisema, makosa hayo yangeweka Vinci Group katika "hali mbaya ya kupata hasara kwa muda mrefu wa kandarasi hiyo, na hivyo basi kuvuruga utekelezaji wote wa mradi huo". Pili, kamati ya uchunguzi ya PPP ilisema KeNHA ilikuwa imefanya kosa kubwa kwa kuruhusu Vinci kutoa zabuni kujibu ya mshindani wake. Kulingana na kamati hiyo, ilichofanya KeNHA ni sawa na "kubadilisha au kuongeza pendekezo la mwenye zabuni", hatua ambayo ni kinyume cha sheria.

Tatu, Dkt Thugge alisema kamati ya uchunguzi ilipata kuwa "kukubali jibu la zabuni kungepatia Vinci ushindani usio wa haki", kinyume cha sheria. Nne, kamati ya uchunguzi ilipata kuwa, "kinyume na uamuzi wa KeNHA kuwa makosa katika kuhesabu ushuru yalikuwa suala dogo", masuala ya ushuru ni ya kisheria, yasiyoweza kupuuzwa. Hatimaye, kamati ya uchunguzi iliagiza KeNHA isimamishe zabuni hiyo, iite kamati ya kutathmini tenda, na kuiagiza izingatie na kujumuisha ripoti na mapendekezo yake. Shirika hilo pia liliagiza KeNHA iwasilishe ripoti iliyofanyiwa mabadiliko kwa Wizara ya Fedha ndani ya siku saba.

Hata hivyo, kwa usaidizi wa wanasiasa wenye ushawishi walioiunga mkono, KeNHA ilishikilia uamuzi wake na kutoa kandarasi hiyo kwa Vinci Group, ikisema tofauti kati ya zabuni ya Kampuni ya Ufaransa na kampuni ya Ureno ilikuwa kosa dogo la kiufundi kuhusu kuhesabu ushuru. Kesi iliyowasilishwa mbele ya jopo la rufaa ya ununuzi na Mote Engil haikufaulu. Wakosoaji walisema huenda Kenya iliingia katika biashara ambayo hatari na kiwango cha hasara hakibainiki. Sehemu tata ya kandarasi hiyo ni suala la "ada za kila baada ya miezi minne" - kiasi ambacho mwanakandarasi atalipwa na serikali kila baada ya miezi minne. Kulingana na mawasiliano hayo, Vinci Group ilitoza Sh5.3 bilioni kila miezi mitatu, huku Mota Engil ikitoza Sh6.2 bilioni, kumaanisha kuwa – kwa mtazamo wa harakakampuni ya Ufaransa ndiyo ilitoza ada nafuu. Lakini baada ya kuhesabu ushuru inayopaswa kulipa serikali kulingana na KRA, malipo yalikuwa Sh4.1 bilioni kwa Vinci na Sh3.9 bilioni kwa Mota Engil - kumaanisha kampuni ya Ureno ilikuwa imetoa pendekezo zuri zaidi.


Inaonekana tofauti katika hesabu ilitokana na matumizi ya lugha ya kiufundi. Kutokana na ukosefu wa uwazi kuhusu jinsi kandarasi hiyo ilitolewa, wataalamu wanasisitiza mradi huo ungeishia kuwa kandarasi isiyo sawa ambayo itahitaji kujadiliwa upya kila wakati kwa kuwa hatari zinazokosa kutambuliwa na kutatuliwa wakati wa kutoa kandarasi hutokea siku za usoni

Ingawa ukweli wa ripoti za vyombo vya habari kuhusu uamuzi wa serikali mpya ya Rais Ruto wa kusimamisha mradi huo haujabainika, mahojiano ya Darubini ya Wiki na wenyeji katika Mamlaka ya Kitaifa ya Barabara Kuu na Idara ya Ushirikiano wa Umma na Kibinfsi ya Wizara ya Fedha (PPP) - mashirika mawili yanayoendesha mradi huo - yalithibitisha kuwa watu wenye ushawishi katika serikali ya Rais Ruto wamezua maswali kuhusu iwapo mradi huo utakuwa na faida yoyote kwa nchi.

Kuna maswali kuhusu mtumiaji kumudu kulipia barabara hiyo huku wakosoaji wakisema ada zilizopendekezwa zitaifanya kuwa ghali sana kwa watumiaji. Kuna malalamishi pia kuwa, kwa sababu kinachopendekezwa ni mfumo wazi wa kutoza ada, watumiaji wa barabara watakaokosa pesa hawatakuwa na njia mbadala ya kuitumia.

Akizungumza na Darubini ya Wiki, mhandisi aliyehusika na shughuli hiyo na afisa mkuu ndani ya serikali mpya walisema kandarasi ya kutoza ada ya barabara ya Nairobi-Nakuru-Mau Summit haifai kwa Kenya na kile sehemu hiyo inahitaji ni barabara mpya kujengwa. Kuna hofu pia kuwa mradi huo ulijadiliwa kwa njia ambayo serikali itakuwa imejiweka katika hatari nyingi.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*




Nation Media Group ©

kurunzi ya kenya

■ MKUU WA MAWAZIRI ATASHIRIKISHA AJENDA YA SHERIA KATIKA WIZARA ZOTE

# MCHAPA KAZI MTEULE WA RAIS

**Rais anatafuta mtu asiye mbishi kutekeleza sera zake, kwa kuzingatia nguvu za upinzani. Uzuri ni kuwa Mkuu wa Mawaziri anapendwa na pande zote mbili**

● NA JOHN KAMAU

Siku 73 baada ya kuunda serikali yake, uamuzi wa Rais William Ruto wa kufafanua baadhi ya majukumu ya Mawaziri huenda ukawa alichokuwa akisubiri Musalia Mudavadi. Kama Mkuu wa Mawaziri, majukumu ya Mudavadi yalionekana kugongana na yale ya Naibu Rais Rigathi Gachagua.


Huku Mudavadi akiwa muungwana mtulivu wa siasa za Kenya, Gachagua mara nyingi ni mtu wa makabiliano. Ingawa Mudavadi, kwa maandishi, ndiye mwanasiasa wa tatu kwa cheo katika serikali ya Kenya Kwanza, Amri ya Rais Nambari 1 ya 2023, inaonekana kumpa nguvu nyingi - zinazokaribiana na zilizokuwa za Waziri wa Usalama wa Ndani Dkt Fred Matiang'I, Rais mstaafu Uhuru Kenyatta alipompa majukumu ambayo, kwa kawaida, yangetwikwa Naibu Rais.

Inaonekana sasa Rais Ruto anamtegemea Mudavadi, mmoja wa wanasiasa wenye tajiriba pana katika Baraza lake la Mawaziri - akiwa katika siasa kwa miaka 34 - akilinganishwa na miaka mitano ya Gachagua kama Mbunge wa Mathira, kuendesha ajenda yake ya uchumi.

Zaidi ya hilo, Mudavadi atasimamia na kushirikisha ajenda ya sheria ya Serikali ya Kitaifa katika wizara na idara zote za serikali, jukumu ambalo litaunganisha afisi yake na ajenda ya chama bungeni. Aidha, atasimamia utelekezaji wa sera za Serikali ya Kitaifa, mipango na miradi, na kumfanya kufika mashinani kiasi.

Jinsi wafuasi wa Gachagua na Mudavadi wanatafsiri mamlaka haya mapya itaelekeza hali ya kisiasa katika muungano huo, ambao unatulia taratibu katika muhula wake wa kwanza. Gachagua anajitahidi kuwa msemaji wa eneo la Mlima Kenya na anataka eneo hilo lenye idadi kubwa ya watu kuungana nyuma yake, hatia ambayo imekasirisha wanasiasa wanaohofia kupanda kwake haraka kisiasa.

Wachanganuzi wa siasa wametambua lugha ya kupalilia ukabila na utamanduni ndani ya eneo la Mlima Kenya, na naibu rais haogopi kujihusisha nayo. Iwapo hilo litatia nguvu chama cha United Democratic Alliance eneo la Kati, au yeye binafsi, inangojewa kuonekana.



Baada ya kuwa Waziri wa Fedha kwa miaka mitano, Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi analeta ujuzi zaidi kuliko siasa.

Ni usawazishaji huu wa kisiasa ambao ulimkabili Rais Ruto - ikizingatiwa kuwa Gachagua bado ni limbukeni katika Baraza la Mawaziri.

Mudavadi, ambaye alikuwa Waziri wa Fedha kwa miaka mitano, analeta ujuzi zaidi kuliko siasa. Anajua jinsi serikali inavyofanya kazi, baada ya kujiunga na Baraza la Mawaziri la Rais Moi akiwa na umri wa miaka 30 na kuhimili siasa za kuchimbana za utawala wa Kanu. Kwa kutegemea Mudavadi, Rais anataka mtu asiye mbishi kuongoza sera zake, ikizingatiwa kwamba kuna upinzani wenye nguvu. Uzuri kuwa Mkuu wa Mawaziri anapendwa na pande zote mbili.

Hivyo basi, Rais anatumia ujuzi ambao Mudavadi amepata kwa miaka mingi – hasa wakati ambao anakabiliwa na uchumi ulio katika hali mbaya.

Mnamo Januari 1993, Rais Moi alikabiliwa na hali sawa ya kiuchumi baada ya kashfa ya Goldenberg ya Kamlesh Pattni na presha kutoka wafadhili. Alimteua Mudavadi, wakati huo akiwa na umri wa miaka 32, kusaidia utawala wa Nyayo kukabiliana na mzozo huo. Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia zilikuwa zimemkaba koo Moi na macho yote yalikuwa kwa Mudavadi kusaidia kutoa Kenya katika mzozo mbaya wa kiuchumi.

Wafadhili walikuwa na imani na Mudavadi na tofauti na wakereketwa wengine wa Kanu - hakuwa na doa. Zaidi, alikuwa miongoni mwa kundi la wanamageuzi walioamini kuwa Kanu na uchumi zingerekebishwa kwa kuleta mawazo mapya, ambayo yangerudisha imani ya wafadhili. Mfumuko ulikuwa umefika kiwango cha juu zaidi cha asilimia 60.

Mudavadi aliruhusu viwango vya ubadilishaji, walivyotaka wafadhili na akaondoa vyeti vya Forex-C, ambavyo vilikuwa vikitumiwa kupitishia pesa wakati wa kashfa ya Goldenberg. Hata hivyo, baadhi ya malipo yalilipwa kabla hajatulia ofisini, na wakosoaji wake wamekuwa wakimlaumu kwa hilo. Pia, alilegeza udhibiti wa bei za mafuta, ngano, mahindi na sukari, akaweka huru uuzaji wa ngano na akaruhusu biashara za utalii kuweka nusu ya mapato yao ya pesa za kigeni. Pia aliondoa mpango wa malipo kabla ya kusafirisha na leseni za uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi.

Waliokuwa na misimamo mikali waliwaita Mudavadi na Ga-

vana wa Benki Kuu ya Kenya Micah Cheserem 'vibaraka' wa IMF.

Kufikia Novemba 1993, Mudavadi alikuwa amerudisha misaada ya wafadhili baada ya kuzimwa kwa miaka miwili. Kenya pia iliahidi kumaliza ufisadi ili ipewe msaada wa dola za Amerika 850 milioni na dola 170 milioni zilizosalia za usaidizi wa malipo. Mojawapo la matukio tata ambayo yalikabili Mudavadi lilikuwa vita dhidi ya wauzaji bidhaa zisizotozwa ushuru walioingiza sukari katika soko la humu nchini. Pia alipata moyo mgumu hasa upinzani ulipojaribu kuvuruga hotuba yake ya kusoma bajeti mnamo 1997 ukitaka mageuzi.

Ni tajiriba hii ambayo Rais William Ruto anataka kutumia na kufanya Mudavadi kuwa mtu wa kupigwa darubini katika serikali hii. Bada ya kukiri kuwa bilionea, Mudavadi anaendelea kupata nguvu katika Magharibi mwa Kenya na ameshusha umaarufu wa Odinga katika baadhi ya zilizokuwa ngome za chama cha Orange Democratic Party (ODM). Hata hivyo, hatua hiyo imezua tumbojoto miongoni baadhi ya wanasiasa wa UDA.

Kwa wiki chache zilizopita, vita baridi – vinavyoendeshwa na washirika wao - vilionekana kushika kasi katika kambi za Gachagua na Mudavadi za serikali ya Kenya Kwanza. Mkutano wa kikazi wa Mt Kenya Safari Club ulikuwa wa kutuliza hali na kulegeza taharuki inayoibuka. Ni kutozima taharuki wakati wa muhula wa kwanza wa utawala wa Mwai Kibaki kati ya chama cha Liberal Democratic party cha Raila Odinga na National Alliance Party of Kenya (NAK) kuhusu ugavi wa mamlaka kulikovunja muungano wa Rainbow Coalition.

Rais Ruto ana kibarua tete cha kusawazisha kwa kuwa Gachagua na Mudavadi kila mmoja anataka mamlaka zaidi. Wote wawili wana azma ya kuwa rais pia.

Kisiasa, Mudavadi ana nafasi kubwa. Atasimamia kamati yenye nguvu ya Makatibu wa Wizara na kusimamia ufuatiliaji wa kiufundi na utathmini wa sera, mipango na miradi ya serikali. Kamati hii inajumuisha walio na mamlaka ya kuagiza matumizi - au 'watu wa pesa' kwa lugha ya mtaa. Pengine kamati hii ndiyo muhimu zaidi katika serikali kwa kuwa hawa ndio wanaoendesha wizara zao tofauti na wanasimamia mabilioni yote zinazotengewa.

Kwa upande wake, Gachagua amekabidhiwa majukumu ya iliyokuwa Wizara ya Ugatuzi na atashirikisha uhusiano wa viwango viwili vya serikali kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti. Pia atasimamia kamati ya Baraza la Mawaziri na kushirikisha washirika wa maendeleo wa kimataifa na Tume mpya ya Mto Nairobi. Rais pia amempa sekta inayotatizika ya kahawa. Baada ya makosa kadhaa ya kisiasa, kurejea kwa Mudavadi kupitia muungano wa Kenya Kwanza kumemfaidi zaidi ya alivyotaka. Ni shughuli ambazo amejua tangu Februari 1989, baba yake, Moses Mudavadi, alipofariki.

Miaka mitano kabla, Mudavadi alikuwa amehitimu kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi na digrii ya uchumi wa masuala ya ardhi. Baba yake alikuwa Katibu Mkuu wa Kanu mwenye ushawishi mkubwa na Waziri wa Moi wa Serikali za Wilaya na Mipango ya Miji. Moi na Mzee Mudavadi walikuwa wamejuana tangu 1949 – na ni Mudavadi, wakati huo akiwa afisa wa elimu, aliyemshawishi Moi kuacha Tambach African School na kujiunga na siasa.



Kutoka kulia: Rais William Ruto, Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi na Naibu Rais Rigathi Gachagua wakati wa mkutano wa majuzi katika Fairmont Mt Kenya Safari Club Nanyuki.
PICHA | MAKTABA

## DOLA 850 MILIONI

**Kenya pia iliahidi kumaliza ufisadi ili ipate msaada wa Dola za Amerika 850 milioni na 170 milioni za kusawazisha biashara yake na mataifa mengine. Moja la matukio tata zaidi lilomkabili Mudavadi ni vita dhidi ya walanguzi wa bidhaa zisizotozwa ushuru waliongiza sukari katika soko la humu nchini.**

**Wiki chache zilizopita, vita baridi – vikiendeshwa na washirika wao - vilionekana kushika kasi katika kambi za Gachagua na Mudavadi za serikali ya Kenya Kwanza. Mkutano wa Mt Kenya Safari Club ulikuwa wa kuzima joto na kulegeza taharuki inayoibuka. Ni kutozima taharuki muhula wa kwanza wa utawala wa Mwai Kibaki kati ya chama cha Liberal Democratic party cha Raila Odinga na National Alliance Party of Kenya (NAK) kuhusu ugavi wa mamlaka kulikovunja muungano wa Rainbow Coalition.**

Kwenye misa iliyofanywa katika Pentecostal Church Valley Road, Mudavadi alijitokeza kama msemaji wa familia. Kwa hivyo ilitarajiwa wazee Wamaragoli walipoita kikao cha wanahabari wiki moja baada ya mazishi na kumuidhinisha kurithi kiti cha ubunge cha Sabatia. Mudavadi alikuwa na umri wa miaka 29.

Punde, wanasiasa wakuu kama aliyekuwa Mbunge Peter Kibisu, walijiunga na wito ulioidhinishwa na tawi la Kakamega la chama cha Kanu chini ya Waziri katika Afisi ya Rais Burudi Nabwera. Mnamo Machi 23, 1989, Musalia alichaguliwa Mbunge bila kupingwa.

Kupitia uchaguzi huo, Musalia alijiunga na siasa bila kizingiti – na pia akapanda hadhi haraka. Miezi miwili baadaye, katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri Mei 1, 1989, yaliyotokana na kujiuzulu kwa Dkt Josephat Karanja kama Makamu Rais na kuteuliwa kwa Profesa George Saitoti, Rais Moi alimteua Musalia waziri wake wa Uuzaji na Masoko.

Mudavadi ameshiriki siasa za kujinusuru pia. Lakini kwa sababu ya upole wake, amekuwa akisalitiwa hata katika ngome yake ya Magharibi. Pia amewahi kufanya makosa ya kibinafsi ya kisiasa. Hata hivyo, wadhifa mpya na majukumu makubwa yanahusu zaidi tabia ya Mudavadi na historia yake. Rais Ruto anaonekana kumwamini.

*jkamau@ke.nationmedia.com @ johnkamau1*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

# habari kwa picha





Mtu aliyeshika mwavuli akipita karibu na duka kubwa la vitabu la Piccadilly la kampuni ya Waterstones akitangaza kutolewa kwa kitabu kwa jina 'Spare' kilichoandikwa na Mwanamfalme Harry wa Uingereza, mjini London, Januari 10. Baada ya miezi kadhaa ya kusubiri na utangazaji, kitabu cha Prince Harry hatimaye kimeanza kuuzwa nchini Uingereza na kutishia aibu zaidi kwa familia ya kifalme. PICHA | AFP



Mkimbizi wa Rohingya atolewa sampuli ili kupimwa virusi vya Covid-19 kwenye makao ya muda eneo la Ladong, Mkoa wa Aceh, nchini Indonesia, mnamo Januari 9. PICHA | AFP



Wakimbizi wa ndani wasafiri kwa trekta na mali zao karibu na kambi ya muda katika eneo lililokumbwa na mafuriko la Dera Allah Yar, Wilaya ya Jaffarabad, nchini Pakistan mnamo Januari 9. Umoja wa Mataifa umetoa wito wa "uwekezaji mkubwa" ili kusaidia Pakistan kufufua uchumi wake kutokana na mafuriko makubwa ya mwaka jana. PICHA | AFP



Nicholas Ireri Kamwende, Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu Mohamed Amin (katikati) wamsindikiza balozi wa Marekani nchini Kenya Meg Whitman baada ya kuhutubia wanahabari katika Makao Makuu ya DCI Januari 12. Balozi alitangaza zawadi ya dola 10 milioni (Sh1.2 bilioni kwa mtu atakayesaidia kupatikana kwa mpangaji mkuu wa shambulio la kigaidi la 2019 katika jumba la dusitD2 ambapo watu 21 waliuawa. SILA KIPLAGAT | NATION



Mwendeshaji baiskeli wa Bolivia Daniel Jager Nosiglia akishiriki shindano wakati wa Hatua ya 10 ya Dakar 2023, kati ya Haradh na Shaybah, Saudi Arabia, mnamo Januari 11. PICHA | AFP



Picha iliyopigwa kutoka angani yaonyesha magari yakipita kwenye barabara iliyofurika katika eneo la Planada, California, mnamo January 10. PICHA | AFP



Waandamanaji wakipinga vibonzo vinavyoonyesha kiongozi mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei vilichochapishwa na gazeti la kila wiki la kejeli la Ufaransa Charlie Hebdo walipoandamana nje ya ubalozi wa Ufaransa katika mji mkuu wa Iran, Tehran, Januari 11. PICHA | AFP

Nation Media Group©

Jukwaa La Vijana



# CHEKA USIKIKE!

*Video cheshi kuhusu maisha ya kawaida za muundaji matini Muchiri Mike katika TikTok zimemletea umaarufu na pesa nzuri*

NAFASI YA VIJANA

## WANAVYOSEMA



**Leslie Osale**

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELB) imenisaidia tangu nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Jomo Kenyatta (JKUAT). Ninaitumia kulipia karo yangu na matumizi ya kibinafsi. Bila hiyo, pengine singejiunga na chuo kikuu au ningeacha shule kwa kukosa karo. Siungi mkono kufutiliwa mbali kwa hazina hiyo. Hatua hiyo itawaathiri vibaya wanafunzi wengi wanaotafuta elimu ya juu.

*- Bw Osale ni mwanafunzi wa JKUAT*



**Annabelle Apondi**

Wanafunzi wanataka maelezo kamili kutoka kwa serikali ya kitaifa kuhusu inavyopanga kushughulikia suala hilo kwa njia ambayo haitawanyima nafasi wanafunzi wanaolenga kujiendeleza kimasomo kutimiza ndoto zao. Kusudi letu kuu ni kubadilisha akili isiyo na chochote kuwa iliyo wazi, hivyo hakuna mtu anayepaswa kuwanyima wanafunzi haki hii asili.

*- Bi Apondi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Multimedia*



**Faith Sudi**

Hatua ya serikali kubuni Baraza la Kitaifa la Kufadhili Ujuzi (NSFC) imepotoka. Kama mtu aliyefaidika na Helb, sijui kama nitalipa mkopo na riba kwani maelezo muhimu, kama vile ni watu gani watafaidika kutokana na hatua hiyo, hayajatolewa. Pili, Helb imenisaidia sana kuendesha maisha yangu chuoni.

*- Bi Sudi ni mwanafunzi wa JKUAT*



**Brenda Gitonga**

Mpango wa kuleta pamoja hazina hizo tatu utaacha wengi katika hali ya kuchanganyikiwa kwani hawana hakina kuhusu matokeo yake. Wanafunzi wengi wamekuwa na wakitumia Helb kulipia masomo na matumizi ya kibinafsi. Kuinama, kauli inayomaanisha kulala njaa, limekuwa neon la kawaida katika vyuo vikuu, licha ya kuwepo kwa pesa za Helb.

*- Bi Gitonga ni mwanafunzi katika Chuo cha Multimedia*

*- Zimetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# Vijana wana ufunguo wa maendeleo barani Afrika

**Mabadiliko ya maisha:** Hili ndilo jambo muhimu zaidi ukuaji, teknolojia ya habari, na mauzo ya bidhaa

• NA SARUNI LEMARGEROI

Wanapotazama siku za usoni za Afrika, wataalamu hutaja idadi kubwa ya vijana wanaoendelea kuongezeka kama rasilimali yake. Kwanza, nusu ya watu wote barani wana umri wa chini ya miaka 20 na mataifa kumi machanga duniani yanapatikana Afrika.

Viongozi wachanga barani Afrika wana manufaa mengine mbali na ukombozi wa kisiasa. Mbele yetu kuna changamoto ya hatimaye kutekeleza suluhisho nyingi ambazo tumezungumzia na kuandika kuzihusu. Mwaka unapoanza, vijana ndio rasilimali kubwa ambayo lazima bara liwekeze na kujiandaa kwa dunia ya kisasa.



Bilas haka Afrika ndilo bara changa zaidi duniani. Asilimia 40 ya watu wake wana umri wa chini ya miaka 15 huku asilimia 20 wakiwa kati ya umri wa miaka 15 na 24. Tungependa kufikiria kuwa hizi ni takwimu za kutia moyo, zinazoashiria kizazi chenye nguvu kinachobuni mustakabali wa bara hili.

Leo hii, hata shahada kutoka chuo kikuu si kigezo cha kupata kazi. Kwa kweli, zaidi ya asilimia 50 ya vijana wa Afrika wanatafuta kazi. Wamesoma, wana mawazo pevu na matamanio makubwa, lakini hayo yote hayawasaidii kupata kazi.

Kufikia 2030, idadi ya vijana barani Afrika inatarajiwa kuwa asilimia 42 ya vijana wote duniani, na asilimia 75 ya walio na umri wa chini ya miaka 35 Afrika. Kukiwa na idadi kubwa kama hiyo ya vijana, sera na mipango itakayoshirikisha vijana katika masuala ya maendeleo inahitajika sana. Kutumia mgao wa idadi ya watu na kupanua fursa kwa vijana - kwa manufaa ya Waafrika wote - kutahitaji data sahihi na ushahidi kuhusu hali ya vijana Waafrika.

Takwimu hizi zinaashiria nguvukazi thabiti kwa miongo kadhaa ijayo. Pia, "mgao huo wa idadi ya watu" unaashiria kundi la viongozi wa baadaye, kutoka jamii za kawaida hadi katika kiwango cha kitaifa. Vijana wanahitaji kazi na kuelekezwa ili waingie katika maisha ya kitaaluma.

Je, Afrika itatumia ipasavyo Uwezo wa ajabu wa watu wake? Huku idadi ya vijana barani Afrika ikitarajiwa kuongezeka maradufu ifikapo 2050, haja ya njia bunifu na endelevu za kusaidia vijana kupata ajira inaendelea kuwa umuhimu. Zaidi ya nusu ya mataifa kumi yanayokua kiuchumi duniani yamo barani Afrika.

Mabadiliko ya idadi ya watu yanatoa fursa ya kuongoza na kushawishi ubunifu ambao utakuwa na umuhimu wa kimataifa. Afrika itaweza kufanya hivyo kama vijana wake wataweza kuongoza maendeleo ya kiuchumi na kuchangia ipasavyo kwa jamii zao.

Ingawa changamoto iliyopo ni ya kutisha, pia imewatia moyo vijana wengi wabunifu na wenye bidii kudhibiti maisha yao ya baadaye, wakibuni suluhisho endelevu ili kujiajiri na kujishughulisha kikamilifu. Viongozi wachanga wa Afrika wanaoendelea kuchipuka wanajumuisha watu wenye matamanio na maono kwa bara hili. Wakishughulikiwa vyema, watahakikisha kila nchi ya Afrika inafaidika kutokana nguvukazi inayoweza kupeleka mbele bara hili.

Afrika ndilo eneo linalofuata kwa maendeleo, ukuaji wa kiteknolojia na mauzo ya bidhaa. Hili limechangiwa na ongezeko kubwa la vijana, ambalo, kando na kuwa kubwa duniani, linatabiriwa kuwa la kudumu zaidi.

Viongozi wa sasa wana jukumu la kushirikisha na kuwakuza vijana wa Waafrika kwa uongozi mahsusi. Ni jukumu la kizazi kikongwe kuhakikisha vijana wamepata elimu bora na ujuzi wa kiufundi, na pia kubuni mwenendo na kujitolea kwa mustakabali wa pamoja wa Afrika.

Baada ya muda, viongozi hao wachanga watatumia ujuzi na tajriba yao kukuza kizazi kijacho. Kwa hivyo, kuwafunza vijana ujasiriamali - jinsi ya kubuni, kuendesha na kusimamia biashara - ili ubunifu na juhudi zao zizae matunda ni muhimu sio tu katika kuimarisha maisha yao binafsi, bali kuimarisha ufanisi wa kiuchumi wa bara zima.

*Bw Lemargeroi ni Msomi katika Mpango wa Mandela Washington, 2019.*

**lemargeroi@gmail.com**

*Una maoni yoyote kuhusu masuala ibuka? Tungependa kusikia kutoka kwako. Tuma maoni yako kwa: weeklyreview@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

Nation Media Group ©

MTAZAMO WANGU



# MAANA HASA YA CRYPTO

**Biashara ngeni:** Pesa zinazowekwa kwa programu ni tofauti na zile wadhibiti wamewahi kushughulikia. Kuzidhibiti kunaweza kuwa changamoto



• NA WAGA ODONGO

Hivi majuzi, Kenya ilitayarisha Mswada unaolenga kutoza ushuru sarafu za dijitali. Mswada wa Masoko ya Mtaji uliofanyiwa mabadiliko, 2022 unalenga kutoza ushuru wabadilishaji na pochi kwa ada kama ushuru wa bidhaa unaolipwa katika kila shughuli ya benki. Mswada huo pia unalenga kukusanya ushuru wa faida ya mali wakati mali ya dijitali inapouzwa. Mswada huo unahitaji watu wanaomiliki au kushughulika na sarafu za dijitali kuripoti wenyewe biashara zao kwa Mamlaka ya Soko la Mali ili watozwe ushuru.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara (UNCTAD) mapema mwaka huu ilikadiria kuwa Wakenya milioni nne wanamiliki sarafu zao za crypto, asilimia ya juu ya wanaozimiliki barani Afrika. Biashara ya ubadilishaji ni kubwa na imegonga kilele chake huku bitcoin ikipanda juu, baadhi ya ubadilishaji ulikuwa wa mali yenye thamani ya Sh10 bilioni kwa wiki.

Pesa tayari zimebadilika kutoka kuwa kidogo na kwa sasa ziko kwa wingi. Taasisi zetu zinazotoa na kudhibiti pesa ni lazima pia zibadilike. Swali kuhusu jinsi ya kudhibiti mali ya dijitali linakasirisha na jinsi sheria hizo zitatekelezwa, kutapelekea hima kunawiri kwa mfumo ambao unatumiwa na mamilioni au zikivurugwa, zinaweza kuua biashara hiyo kabisa.

Suala la kwanza ambalo wabunge wanahitaji kuwazia ni jinsi ya kuainisha aina tofauti za mali. Tunashughulika na maelfu kadhaa ya sarafu, na yeyote aliye na ufahamu mdogo wa kutayarisha programu anaweza kuunda sarafu kwa chini ya saa.

Muungano wa Ulaya ambao umepiga hatua katika mchakato wa udhibiti umegawa sarafu hizo mara nne: Mali, tunu za matumizi, sarafu imara na pesa za elektroniki.

Ingawa unaweza kutengeneza pesa kutoka kwa mali kama bei ya Bitcoin kupanda, huwezi kunufaika na ongezeko la bei katika sarafu imara kwa sababu bei yake inaweza kukitwa kwenye mali halisi ya ulimwengu ambayo bei yake haishuki.

Basi tunahitaji kuamua ni mali gani inayopaswa kutozwa ushuru wa mauzo, na ni gani ya kutozwa ushuru wa faida. Chukua mfano wa altcoin inayopendwa sana duniani Ethereum: kwa kuifanya thabiti, kuongezeka kwa bei kunaweza kuchukuliwa kuwa kuvutia ushuru wa mauzo ya mali, wakati inabadilika kuwa hisa - ambapo umiliki wake unaamua anayepata zaidi - na anapata mgao.

Kitu kingine cha kuzingatia ni jinsi ya kushughulikia masuala yanayohusu huduma za ulinzi wa mali ya dijitali. Je, funguo za ubadilishaji nchini zinafaa kuwa nchini humo? Kufanya hivyo ni muhimu kwa sababu itaruhusu serikali yetu kulinda watumiaji iwapo ubadilishaji utaporomoka.

Njia moja ya kutatua hili ni funguo zihifadhiwe nchini au aina fulani ya hifadhi ya mali inayohusika iwekwe na shirika la serikali. Jinsi hili litatekelezwa hapa Kenya haijulikani.

Jinsi ya kueleza hasa vile mali inauzwa pia itakuwa muhimu iwapo tutahesabu ushuru. Mabadiliko ya bei ya asilimia kumi ndani ya siku chache ni jambo la kawaida. Kwa kuwa shughuli nyingi za ubadilishaji hazifanyiki katika mfumo mkuu wa mali ya dijitali, kuna wasiwasi kwamba nyakati halisi ambazo mali huuzwa zitafichwa kusadifiana na hasara ya kuanzia asilimia kumi.

Wanaweza kuwa wajinga wakikosa kufanya hivyo kwa kuwa ni vigumu kuwapata wakidanganya. Pengine hii ndiyo sababu Mswada utakuwa ukitegemea wamiliki kuripoti wenyewe - ni vigumu sana kubaini shughuli bila kushirikisha wamiliki.

Mfumo wote kama unavyopendekezwa kwa wakati huu, utategemea ukarimu na uaminifu wa umma. Masoko ya hisa yananapaswa kuweka siri kuu matumizi ya data.

Swali lingine la kuwazia ni kuhusu mahali mabaki ya sarafu imara yatawekwa. Je, yanafaa kuwekwa katika Benki Kuu kama zinavyofanya benki za kawaida? Bila shaka hili itasaidia kuwa thibitisho la hifadhi zilizopo.

Usimamizi wa sarafu imara zinazopatikana humu nchini utakuwa vigumu kwa wabadilishaji wa kimataifa kwa kuwa zinaweza kutwaliwa kiholela.

Ni muhimu kujibu swali hili kwa kuwa kwa wakati huu soko kubwa sio lililo na wabadilishaji wa bitcoin kadhaa, ni soko la sarafu imara. Kwa Wakenya wengi, sarafu za dijitali ni suluhu kwa wanachohisi kuwa usimamizi mbaya wa pesa na CBK badala ya kubahatisha ili kupata faida.

Ukihitaji watumiaji wanaofanya biashara nchini kuwa na nambari ya KRA, utakosa sehemu kubwa ya soko. Hatua kama hiyo itafanya watu wengi kuamua kutumia mitandao ya kibinafsi ili wasijulikane waliko.

Wauzaji wakubwa katika masoko yanayohusiana ya humu nchini si Wakenya. Hii pia itafanya sarafu za dijitali kuwa ghali Kenya, jambo ambalo litafaidi wamiliki na matajiri ambao wanaweza kuhamisha pesa kati ya maeneo ya usimamizi.

Ukweli ni kuwa pesa zinazoweza kuwekwa kwa programu ni tofauti na chochote ambacho wadhibiti wa soko au benki kuu wamewahi kushughulikia.

Ni changamoto kuzidhibiti. Ushauri wangu wa bure kwa bunge ni kuketi kitako, kupuuza biashara hiyo na kusubiri Ulaya, Singapore na Amerika kuunda sheria zao, kisha liazime mawazo mazuri.

*Bw Odongo mhandisi wa Programu. wagaodongo@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group ©

UUNDAJI PESA KUPITIA MITANDAO YA KIJAMII

# NI KICHEKO TU!

**Video za uchesi kuhusu maisha ya kawaida za muundaji matini Muchiri Mike katika TikTok zimemfanya maarufu sana na zinamletea pesa**

• NA EDDY ASHIOYA

Ukweli wa ucheshi: Muchiri Mike yumo kwenye Facebook. Nani? Yule jamaa wa TikTok, anayeigiza kina mama Waafrika (Mama Mike), walimu Waafrika na mtu mwingine yeyote, bila shaka. Unamjua.

Lakini huko nyuma kuna uovu unaonyemelea: Kwamba Muchiri Mike (sio 'Mike Muchiri', au 'Mike') anakaribia kufikia kiwango cha umaarufu cha kulipia.

Hizi si habari nzuri sana kwa mashabiki wake wa dhati, nikiwemo, ambao wamefurahia matini yake kwa miaka mingi lakini wakaihifadhi kama kitu kitakatifu. Tulikuwa kundi dogo lenye lakini tulipenda usiri wetu. Yamkini Muchiri Mike aliupenda pia; hakuwa na haraka ya kuwa katika kila jukwaa maarufu, ni kijana tu aliyekuwa akifanya mambo yake, na kufurahia.

Sasa je? Kila mtu anataka kipande cha Muchiri Mike. Ufanisi wake umetokana na kupendwa kwa matini yake katika TikTok, ambapo, ambapo maisha ya kisasa na masuala ibuka huigizwa kwa njia ya kuchekesha. Video yake ya majuzi (kufikia wakati wa kuchapisha makala haya) ilikuwa imevutia mamilioni ya watu (watu 3.9) na mamia ya video za kuigwa na akaunti feki. Katika video hiyo, (utashangaa!) anajifanya bikizee anayepokea simu ambazo wewe huenda umepokea pia, matapeli wanaokwambia wamekutumia pesa kimakosa. Unafurahia jinsi anawazungusha huku na kule na kushinda ujanja wao huku akituacha, sisi hadhira yake mateka, tukiumwa na mbavu kwa kicheko.

Huyo ndiye Muchiri Mike. Ni kijana mwenye umri wa miaka 24 anayezungumza kwa lafudhi ya kijana-mpole-kutoka-milimani. Lakini unahisije kuwa Muchiri Mike? "Ni ajabu. Wakati mwingine huwaonea wivu watu ambao sio mimi. Kwanza, Muchiri Mike ana kipaji kikubwa. Ameumbwa akaumbika. Nafurahia kiwango cha maisha yangu kwa sasa. Nahisi vyema sana kuwa Muchiri Mike."

Na kufikiri amekuwa kwenye mtandao wa TikTok kwa mwaka mmoja tu na mabadiliko yote hayo! Kitindamimba wa familia ya watoto watano (kaka watatu, dada mmoja), anakumbuka safari yake ya umaarufu ilianza mapema kuliko TikTok. "Nilianza kubuni matini katika Facebook na Instagram. Facebook ndiyo ilikuwa jukwaa langu la kwanza na ndipo nilianza kupata idadi kubwa ya hadhira inayotazama video zangu.

Watu zaidi 300,000 waliokuwa wakifuatilia matini yake wakati huo walikuwa wengu sana. Kuingia kwake polepole katika TikTok kulikuwa hatua ndogo ya ufanisi mkubwa – aligonga kilele katika jukwaa hilo mapema mwaka huu. (Wengi wa wateja wangu sasa wanataka nitume matini yangu kwa TikTok. Na wakati mwingine katika Instagram."

Huenda nyota yake haikuwa hapo, lakini ilikuwa imebatizwa. Sawa inavyokuwa mara ya kwanza, video ya kwanza ya Muchiri Mike katika TikTok haikutia fora. Ilikuwa pia mara yake ya kwanza kuigiza wanawake.

Lakini katika fikra zake, kulikuwa na mseto wa hisia. "Sikuwa na hakika. Unajua, watu watafikiria nini? Zilikuwa fikra za kutisha. Sana. Watu 500 ndio walikuwa wakitazama video zake alipiongia TikTok – idadi ambayo bado ni kubwa kwa mtu mwingine yeyote huko nje - lakini hilo lilimfanya ajiondoe, ingawa kwa muda mfupi. Alirudi Machi 2021. TikTok sasa ndiyo jukwaa lake maarufu zaidi, huku watu wengi wakimtambua kupitia hapo. TikTok inauza kwa sababu matini yake maalumu haitegemei marafiki zako kutangamana na kuburudika ila kwa "mapendekezo" – jambo linaloifanya kuwa rahisi kupata umaarufu katika jukwaa hilo.

Umaarufu wake, unatokana na kuwa kaka wa kila siku anayegeuza mambo ya kila siku katika maisha ya kawaida kuwa video 'zinazohusiana' na hadhira. Na pia, jambo ambalo mashabiki wake wa kike watakubali, ni wazi kuwa Muchiri Mike ana maumbile ya kuvutia



**Muchiri Mike ni muundaji wa matini za TikTok na mcheshi, maarufu kwa jina la uigizaji 'Mama Mike'. Alishinda tuzo ya 2022 ya Mshawishi Bora wa Mwaka.** PICHA | EDDY ASHIOYA

Nation Media Group

sana kama mwanamme, hasa tabasamu lake. Je, anajua anatatiza watu wengi wenye kumbukumbu ya kiwango cha juu – na sizungumzii kunihusu mimi? "Labda kwa kuwa kila mtu alilelewa na mama asili wa Kiafrika. Huenda katika maisha yangu mengine nilikuwa mwalimu au mama Mkenya.

Lakini pia nafikiri mimi ni mtu mwenye makini kwa mambo." Anaturudisha nyuma enzi zake shuleni, ambapo anakumbuka kuwaigiza walimu wake, hasa wanawake. Maswali zaidi, anakumbuka zaidi, kumhusu akiwa katika shule ya msingi, akifanya mzaha, mtoto mcheshi mwenye furaha, ambaye hungetaka kusimama karibu naye mwalimu mkuu alipokuwa amekasirika. Waswahili husema: "Wali wa kushiba huonekana kwenye sinia."

Talanta yake ya kipekee inampa riziki. "Juzi nilishirikiana na Safaricom kutangaza Apu ya M-pesa. Na usifikiri ni Safaricom tu. Wateja wake wakuu wanajumuisha Netflix (kutangaza shoo ya Afrika Kusini inayoitwa Savage Beauty), Juicy Fruit, Baygon, IEBC, Coca Cola (kutangaza Kombe la Dunia la FIFA) miongoni mwa wengine. Anatumia neno ushirikiano badala ya "kufanyia kazi fulani au kufanya kazi na." Kwa nini?

"Mteja akinielezea anachotaka ninawapa nakala na tunaamua kinachoridhisha hadhira zetu sote. Ni ushirikiano na ubunifu wa pamoja."

Hivi majuzi, aliigiza kama mhusika mkuu katika Too Early for Birds, mchezo wa kuigiza katika ukumbi wa Jain Bhavan, Loresho. "Nilikuwa nikishirikiana katika mradi fulani na Queen Gathoni, ambaye ni mmoja kati ya wenye shoo hiyo.

Alinieleza alichokuwa akifanya (mchezo huo) na alitaka nishiriki." Lakini haijawa hivi kila wakati. Kazi ya kwanza aliyowahi kupata ilikuwa 2017 – mwaka mmoja baada ya kuanza kubuni matini. "Nilishirikiana na nembo na wakala wake akachukua muda mrefu kunilipa."

Malipo yake wakati yalikuwa Shs100,000. Bila shaka ada zimeongezeka. Sana."

Sifa, anasema, imeathiri vibaya maisha yake kijamii. Au kuyakosa. Ananiambia hawezi kutembea barabarani bila mtu kutaka wapigwe picha. Au utani? Anacheka. "Watu hufikiri mimi ni mchangamfu sana lakini huenda si kweli. Wakikutana nami huko nje na kupata wasichotarajia, unajua, ni shida."

Anatamani siku ambazo angeenda popote bila kofia wala barakoa. Mtu wa kawaida tu na shughuli zake mjini.

"Mimi ni mtu mwenye hulka zote. Ninakuwa mchangamfu ninakikutana na watu ninaowafahamu. Katika mazingira mapya, ninashindwa kutangamana na watu."

Watu humtarajia kupaaza sauti huko nje. Lakini ni mtulivu sana. Wanaoweza kukerwa na nafsi yake watasononeka kufahamu kuwa, kama mtu binafsi, ni mcheshi, mwenye kuburudisha na mtu wa kuvutia sana. Lakini umaarufu umempa nini? "Mungu wangu! Anasema. "kuna manufaa chungu nzima ya kuwa mtu maarufu." Anazungumzia nembo za bidhaa ambazo ameshirikiana nazo na hela ambazo zimejaza mifuko yake. Amehamia nyumba mapya, akaoa na hivi majuzi alinunua gari. "Sifa bila shaka imekuja na mazuri."

Muchiri Mike, ambaye alisomea Sayansi ya Matibabu katika Chuo Kikuu cha Daystar sasa anajitambulisha kuwa muundaji matini. Inamchukua nusu siku kukamilisha matini yake.

"Kurekodi video hakuchukui muda mwingi." Bila shaka haichukui muda mrefu ukiwa mweledi wa aina yake, kipaji adimu sana, mwanamme mwenye vipaji vingi kama yeye. "Kuhariri ndiko kuliko na kazi nyingi."

Nashangaa iwapo wakati mwingine anahisi kwamba anachukuliwa ama kuonekana kuwa aina fulani ya muundaji matini, mchekeshaji na mwigizaji wa zamu. Hasa, Muchiri Mike anajichukulia zaidi kuwa mwanamuziki kuliko muundaji matini. "Katika siku za hivi karibuni, nitazindua maigizo ya injili yaliyo na nyimbo saba au nane. Ni mradi ambao nimekuwa nikiufanyia kazi tangu mwanzo wa mwaka huu. Mojawapo la malengo yangu makuu mwaka wa 2023 ni kumakinika kuhusu muziki wangu.

Anamtaja Mungu mara kadhaa katika mazungumzo yetu. Alilelewa katika familia ya Wakristo sugu. Mungu daima alikuwa kwenye



## KIONGOZI WA IBADA

Muchiri Mike aliteuliwa Mshawishi Bora wa Mwaka wa 2022 na kampuni ya was va Digital Media Awards Kenya.

Alianza kuunda matini katika mwa 2017, akiegemea visa vya kawaida ili kuleta kumbukumbu na vituko vyautotoni

Ana wafuasi zaidi ya 300,000 kwenye majukwaa yote anayotumia.

Muchiri Mike pia ni kiongozi wa ibada, MC wa mashirika na mwimbaji wa nyimbo za injili.

meza ya chakula cha jioni, kichwa cha familia. Ilikuwa kawaida kwa familia nyingi za Kiafrika kulelewa ukihudhuria shule za Jumapili. "Siku za Jumapili zilikuwa za kwenda kanisani. Kama hukutaka kwenda, ulikuwa unapata jibu la kawaida la mama Mwafrika, "Toka basi nifunge nyumba yangu" Alichukia sana alfajiri za Jumapili lakini alipenda zaidi nyimbo za sifa na ibada kanisani.

Hivyo basi, Mungu, ni nani kwake? "Mungu ni Mungu kwangu. Ninamwamini Mungu. Na kutokana na tajiriba zangu binafsi, nimelazimika kumtafuta Mungu kibinafsi na kumfahamu kwa namna yangu mwenyewe." Mimi si malaika, anasema, ni rahisi kumkosea Mungu.

"Hatimaye, kilicho muhimu uhusiano wako na na Mungu wako." Hataki kugeuka mhubiri, anasema. Lakini ni muhimu kumsikiza. Hakuna anayefahamu hadithi yako vyema kukushinda wewe mwenyewe, kwa njia bora zaidi kuliko Mungu anavyoifahamu. Anarudi kwa mawazo yake, akizingatia imani yake: kile ambacho Mungu anaweza kuwa kwake. Kile ambacho yeye binafsi anaweza kuwa kwa Mungu.

Wazazi wake wanafikirta nini kuhusu matini yake? "Wananiunga mkono kwa dhati. Kwa kweli, baba yangu huweka baadhi ya video zangu kwenye safu yake ya WhatsApp na huwa nashangaa na kumuuliza, ulipata wapi hiyo?" Kama maisha yangekuwa filamu, nani angeigiza nafsi yake? "Dada yangu ananijua vyema kabisa. Anaweza akaigiza kila kitu jinsi kilivyo kabisa. Ni yeye tu anayeweza kuigiza nafsi yangu."

Kazi yake, inaonekana, ni kuwafurahisha watu. Lakini ni lini mara ya mwisho aliweza kuangua kicheko hicho cha dhati? "Nimekaa kwa muda mrefu sana. Pengine tulipokuwa tunafanya mazoezi ya Too Early for Birds na Esther (Kazungu). Hiyo ndiyo mara ya mwisho niliangua kicheko cha dhati."

Je, mtazamo wake kuhusu pesa umebadilika? Anasimulia jinsi familia yake ilivyoishi maisha mazuri yakifuatiwa kipindi kirefu cha ufukara. Nadharia ya Yusufu – si unajua, miaka saba ya shibe ikifuatiwa na miaka saba ya njaa katika Kitabu cha Mwanzo.

"Kwa bahati mbaya, nilizaliwa wakati wa kipindi cha umaskini. Ndugu zangu kwa kweli walifurahia pesa. Mara tu nilipozaliwa, mambo yalibadilika ghafla na tulilazimika kuzoea maisha mapya."

Hali hiyo iliathiri jinsi anavyotangamana na pesa. Anakumbuka jinsi, hapo awali, angepanga bajeti kali na kuwajibikia kila shilingi. "Sasa mimi ni mtumiaji anayewajibika, lakini pia huwa sijisumbui sana kuhusu hela." Hata hivyo, anasisitiza niandike kuwa hapati mamilioni. Ni kwamba tu ameridhika, licha ya wazazi wake kufikiri kwamba ni tajiri mkubwa. "Mimi bado ni mtoto. Mtoto wao. Mimi bado ni watoto!" Huwa hasemi tu vitu vya kuchekesha, huwa anasema vitu kwa namna ya kuchekesha.

Nyakati kama hizi unaona talanta yake, jambo ambalo limemweka jukwaani, moja kati ya sifa zake za kuvutia, inayoonyesha jinsi alivyo mtu wa kuvutia, kijana wa kawaida kutoka kijiji cha kawaida ambaye tu amebarikiwa mno na ni mcheshi. Siri yake ni nini? Ni mwerevu au ni bahati tu? "Mimi ni mwerevu asilimia 100. Hilo, na Mungu.

*eddieashioya@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

UTALII NA USAFARI

# ANAUNDA MAMILIONI KUTOKANA NA UTALII

**Akitambuliwa kuwa mmoja kati ya viongozi vijana wenye ushawishi mkubwa duniani, Steve Nuguti anajenga biashara kubwa ya uchukuzi na kuwapa vijana nafasi ya kustawi katika sekta hiyo**

• NA SINDA MATIKO

Baada ya kupiga gumzo na mlinzi usiku kucha kwa kukosa nauli ya kumwezesha kurudi nyumbani baada ya kazi ngumu ya mchana kutwa, Mark Steve Nuguti anaelewa maana ya mtu kulala njaa jijini Nairobi.

"Nairobi ni shamba la mawe, ndugu yangu. Unapaswa kuwa na moyo wa chuma kuishi jijini," anasema kwa tabasamu lenye utundu fulani, tunapokutana katika afisi yake katika orofa ya nne ya jumba la Ngong Lane Plaza.

Siku ambayo hangweza kurudi nyumbani alikuwa akiishi katika mtaa duni wa Githurai 45 viungani mwa jiji na alifika jijini kila siku kutafuta kazi za afisi, na wakati mwingine kazi duni za kibarua.

"Nilihitimu mnamo 2010 kutoka Chuo Kikuu cha Mount Kenya, Thika, ambako nilisomea Usimamizi wa Masuala ya Utalii. Kuwa mhitimu wa chuo kikuu asiye na kazi jijini ni maisha machungu. Hiyo ilikuwa miaki migumu zaidi katika maisha yangu," anakumbuka.

Sasa, mwanamume huyo wa umri wa miaka 32 ni miongoni mwa mamilionea wenye umri mdogo zaidi nchini Kenya. Mwaka jana, alisherehekewa katika Umoja wa Milki ya Kiarabu (UAE) na kutunukiwa tuzo ya Kiongozi wa Vijana wa Mwaka mwenye Ushawishi Mkubwa, wakati wa Kongamano la Wakfu wa Uongozi wa Vijana Afrika jijini Dubai.

"Ilikuwa heshima kubwa kupewa tuzo hiyo na Mstahiki Sheikh bin Majid Al Muall na kuorodheshwa miongoni mwa watu 50 wenye ushawishi mkubwa duniani," anasema Steve.

Steve anayeongea kwa upole na ufasaha, ni mchapa kazi. Sasa halali njaa, labda kwa kupenda, anavalia mavazi anayotaka na huendesha magari ya kifahari. Kila nyota inaonekana kumwangazia. Amejijengea himaya na anaazimia kusaidia vijana wenzake.

Wakati fulani alikuwa ameajiriwa, lakini sasa Steve ameajiri watalaamu 15 wenye umri mdogo katika kampuni yake ya uchukuzi wa watalii, Spoton Vacation, aliyoanzisha miaka miwili iliyopita.

"Mfanyakazi wangu mwenye umri mkubwa zaidi ana miaka 35 na wengi wao ni wanawake wenye umri wa kati ya miaka 20 na 30. Lengo langu ni kuwakuza na kuwasaidia kwa njia bora niwezavyo katika sekta hii," anasema. Steve anasisitiza kuwa hatang'ang'ana kudumisha hata wafanyakazi wake wazuri zaidi wakitaka kuondoka Spoton Vacation kwenda kwingineko.

"Kuna haja gani ya kumkuza mtu fulani kama hutawaruhusu kujiendeleza katika taaluma yake? Tunahitaji kuzalisha vijana wengi mamilionea jinsi tunavyoweza. Ni faida kwa jamii," anaeleza.

Safari yake katika sekta ya utalii ilianza miaka 15 iliyopita, alipoanza kuhudumu kama mshauri katika masuala ya kuvutia watalii, kisha akajiunga na uvumishaji na hatimaye uuzaji huduma za kampuni. Alifanya kazi katika kampuni nne za kitalii kabla ya kujiunga na Bonfire Adventure, ambako alitawazwa kuwa Meneja Bora wa Mwaka mara kadhaa.

Anajivunia kustawisha Bonfire Adventure, inayomilikiwa na Susan na Simon Kabu, ambao sasa ni washindani wake, kampuni maarufu iliyofaulu kupitia mikakati yake ya uvumishaji.

"Nilifanya kazi nyingi nikiwa huko na nina uhakika wenye kampuni hiyo wanaweza kuthibitisha hilo. Niliondoka baada ya miaka mitano, kampuni hiyo ilipokuwa kileleni cha ufanisi wake, na kuanzisha kampuni yangu. Ujuzi wa miaka kumi ulitosha kunifanya kuwa Afisa Mkuu Mtendaji," anasema Steve akicheka.

Ilikuwa kazi ngumu kuanzisha Spoton. Lakini Steve alipewa motisha na ndoto ya kuwa Afisa Mkuu Mtendaji; hangerudi nyuma. "Nilikuwa tayari kuanza biashara yangu. Nilijua jinsi ya kuendesha biashara hiyo kwa sababu ya ujuzi niliopata miaka ya nyuma. Ku-




Mark Steve, Mwanzilishi na Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya Spoton Vacation.
PICHA | TOMAS MATIKO

Nation Media Group



**Watalii katika hoteli ya Leopard Beach Resort eneo la Diani, Kaunti ya Kwale, mnamo Desemba 22, 2022. Kufikia mwisho wa 2022, Spoton Vacation ilikuwa imepeleka wateja zaidi ya 1,000 sehemu za humu nchini na kimataifa, ilhali wengine 400 walilipa dola nyingi kupelekwa Italia, Ufaransa na Ubelgiji.** PICHA I SIAGO CECE

husu pesa za kuanzisha biashara, nilikuwa nimeweka akiba ya mamilioni kwa miaka kadhaa kwa ajili ya kuanzisha kazi kama hiyo."

Spoton ilipoanza kutoa huduma Steve alitegemea wateja wengi aliowahi kuhudumia na kuanzisha ushirikiano nao. "Mwaka wa kwanza haukuwa wa kutengeneza faida lakini wa kujenga biashara. Nilianza kwa kuajiri mtu mmoja na kuongeza jinsi nilivyohitaji. Lengo langu ni kuajiri watu wengi niwezavyo." anaeleza.

Licha ya kuwa katika biashara hii kwa miaka mitatu, na uwezo wa kifedha wa mamilioni, Steve anashikilia kuwa biashara yake bado ni changa. "Pesa hizo hurudishwa kujenga biashara hii, kwa hivyo sizioni kama faida kufikia sasa. Faida ni suala ambalo tunaweza kujadili baada ya muda wa miaka mitano," akasema akicheka tena.

Kufikia mwisho wa 2022, kampuni ya Spoton Vacation ilikuwa imesafirisha wateja 1,000 katika maeneo mbalimbali nchini na kimataifa huku wengine 400 wakilipa dola kadhaa kupelekwa kutalii nchi za Italia, Ufaransa na Ubelgiji. "Tunatoa nafasi hii kwa kila Mkenya. Tuna huduma ambazo zitafaa kila mtu. Ziara za kupumzika si za matajiri pekee; hiyo ni dhana ambayo Spoton inataka kuondoa. Tunatoa huduma zinazogharimu pesa kidogo kiasi cha hadi Sh2,000 za kuzuru maeneo mbalimbali humu nchini.

Anapenda wapi zaidi? "Hilo ni swali gumu kujibu," akajibu. Nimesafiri kote duniani na kuna sehemu nyingi nzuri kutalii, lakini nikilazimishwa kuchagua, nitasema Kenya na Morocco.


*tmatiko@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*




Nation Media Group©

maoni




■ Rais hapaswi kuwa na mamlaka makubwa kiasi cha kukataa maamuzi ya watu ghafla

# Waliokataliwa hawafai kuwa mawaziri



KWENDO
**OPANGA**

Nilipokuwa nikitazama picha kutoka kwa kikao cha Mawaziri na magavana mjini Nanyuki,

sikuweza kujizuia kushangaa kuhusu maana halisi ya nguvu ya raia dhidi ya maagizo ya Rais. Miongoni mwa mawaziri wa Rais Ruto ni watu waliokataliwa na wapigakura wakati wa uchaguzi lakini baadaye wakateuliwa katika Baraza la Mawaziri.

Na kuna Mawaziri waliopigiwa kura na wananchi kuwa wawakilishi wao katika Mabunge yote mawili lakini Rais akawateua kuhudumu serikalini. Hatua hiyo iliwafanya wapigakura kurudi tdebeni kuchagua watu wengine kuwa wawakilishi wao katika Bunge.

Wapigakura wanasema hawataki watu fulani kuwa wabunge. Hiyo ina maana kwamba hawawataki watu hao kuwawakilisha, kufuatilia utendakazi wa serikali au kutengeneza sheria.

Watu hao wanashindwa, lakini Rais anasema ni sawa tu, nitawaingiza serikalini. Wanaokataliwa na raia, Rais anawateua.

Kisha, wananchi, kwa kutumia uwezo wa kura unaowawezesha kuteua na kufukuza, wanateua wawakilishi wao katika Bunge, lakini Rais anaingilia tena. Anaamua wananchi hawajawachagua watu wanaofaa kuwatungia sheria na kuiwajibisha serikali. Hivyo, anawateua hao serikalini kuendesha ama kutekeleza yanayopitishwa na Bunge.

Kwa hivyo, wanaochaguliwa na watu, Rais anawakataa. Mtu ambaye wananchi wanasema anafaa kuwajibisha serikali, Rais anasema badala yake, anafaa kuwajibishwa, hivyo, tafadhali sasa chagueni mtu anayefaa kuiwajibisha serikali. Na, tafadhali fanyeni hivyo kutoka kwa mapato yenu; ndiyo, pesa zenu. Ahsanteni sana. Unakumbuka kitu? Watu waliokataliwa na wapigakura ndiyo washirika wa karibu wa Rais, wapambe na washawishi wa aina mbalimbali. Na watu waliochaguliwa na wapigakura pia ni washirika wa Rais, wapambe na washawishi wa aina mbalimbali.

Jambo lingine, Katiba inasema nini kuhusu ujumuishaji wa Mawaziri? Kwamba hawatakuwa Wabunge.

Kwa wengi wetu, hili lilimaanisha Mawaziri hawatakuwa wanasiasa. Hili, kwa wengi wetu lilimaanisha Mawaziri wangekuwa wanataaluma. Na kwa wengi wetu, hili lilimaanisha kuwa siasa zingeondolewa katika Baraza la Mawaziri ambapo shughuli kuu ya serikali ingekuwa kuwatumikia raia, kutimiza ahadi za uchaguzi na manifesto.

Mnamo 2013, hali ilionekana kuwa hiyo. Walivaa mavazi yaliyofanana. Rais na Naibu Rais waliwapa Wakenya wanataaluma kama Mawaziri. Lakini baada ya siku kadhaa, wanasiasa walitajwa kuwa mawaziri, huku Ruto, wakati huo akiwa Naibu Rais, akitangaza kuwa kungekuwa na wanasiasa wawili tu katika Baraza la Mawaziri, yeye na Rais.

Hilo lilimaanisha kuwa wanasiasa waliotangazwa Mawaziri, yaani Charity Ngilu na Najib Balala, wangejiondoa siasani na kugeuka kuwa wanataaluma.

Nafasi nzuri. Baadaye alifuatia Mwangi Kiunjuri na uvumi uliokuwepo ni kwamba ilikuwa vigumu kwa Rais na Naibu Rais kuendesha serikali bila ya wanasiasa kukabili upinzani ambao ulikuwa ukiwaelekezea kila aina ya shinikizo katika kuiwajibisha serikali.

Mnamo 2018, kulikuwa bado na hali ya hadaa. Mpango wa Kubadilisha Katiba (BBI), mchakato wa kisiasa ulioendeshwa na Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani, Raila Odinga, ulipendekeza mageuzi ya kikatiba, baadhi yakiwa kuruhusu Baraza la Mawaziri kuundwa kutokana na Wabunge. Baraza hili la mawaziri halijumuishi wanasiasa kwani wanasiasa hao walijiuzulu kutoka kwa nyadhifa za kisiasa.

Baraza hili halijumuishi wanasiasa kwa sababu wanasiasa hao walikuwa wameshindwa kwenye chaguzi kabla ya kuteuliwa kuwa Mawaziri. Upuuzi mtupu.

Rais hapaswi kuwa na mamlaka makubwa kiasi cha kukataa maamuzi ya watu ghafla.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

maoni

■ SHERIA YA UONGOZI NA MAADILI

# EACC inahitaji vitendo kupigana na ufisadi



MACHARIA **GAITHO**

Kwa mzaha huu na mingine, tafadhali tembelea tovuti eacc.go.ke. Hilo ndilo jambo la kwanza nililowaza baada ya kubaini Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi (EACC) inashinikiza kuwepo kwa sheria inayolazimu watu wote wanaotafuta kazi katika utumishi wa umma kupita mitihani ya uadilifu.

Kama Afisa Mkuu Mtendaji wa EACC Twalib Mbarak (pichani), mwenyekiti Askofu Eliud Wabukala na makamishna wenzao hawajatua nchini kutoka sayari ya Mars), watajua kuwa pendekezo kama hilo haliwezi kupita katika bunge linalodhibitiwa na muungano wa Kenya Kwanza.

Huenda EACC ina nia nzuri, lakini ni wazi haikutafuta ushauri kabla ya kupendekeza wajibu wa kuwachunguza wanaotafuta kazi katika utumishi wa umma.

Hata kabla ya mageuzi yanayopendekezwa ya Sheria ya Uongozi na Uadilifu kuwasilishwa rasmi, tayari, Kiongozi wa Wengi katika Bunge la Kitaifa Kimani Ichung'wa, anayapuuzilia mbali. Ichung'wah, ambaye ni Mbunge wa Kikuyu, ni mfuasi sugu wa utawala wa Kenya Kwanza ambaye tayari amesahau ni mwanachama wa Bunge, tawi huru linalopaswa kukagua utendakazi wa serikali. Anajiona kuwa afisa mkuu katika uongozi wa chama na pia kama mwanachama wa Serikali.

Bila shaka atashinikiza msimamo wa chama bila kuuliza swali, ambapo ukosefu wa maadili, mashtaka ya ufisadi na makosa mengine ya jinai yanaonekana kuwa kigezo cha kufaulu kwa anayetafuta cheo cha umma.

Tume ya EACC imejaribu iwezavyo kukabiliana na ufisadi, angalau ikilinganishwa na idara nyingine za serikali. Haikujiingiza katika kashfa za mashtaka ya kisiasa ambazo zimezipaka tope Idara ya Kuchunguza Uhalifu (DCI) na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP).

Kinyume na idara hizo mbili, haijakubali kutishwa kisiasa - baada ya serikali mpya kuchukua mamlaka mamlaka - kuondoa mashtaka ya jinai dhidi ya washirika wa chama hicho yaliyokuwa yamewasilishwa na utawala uliopita bila ushahidi, kwa manufaa ya utawala huo.

Lakini shirika hilo limekuwa kama mbwa asiye na meno. Ndilo shirika rasmi lililobuniwa na sheria kuongoza vita dhidi ya ufisadi, lakini lilikaa kimya majukumu yake yalipovamiwa na kuchukuliwa na DCI na DPP, waliokuwa wakiendesha mashtaka yaliyofunguliwa kisiasa.

Tume ya EACC pia imekuwa bure katika kushinikiza utekelezaji wa Sheria ya Uongozi na Maadili na Sura ya Sita ya Katiba kuhusu Uongozi na Maadili.

Mnamo 2013, ilipoamuliwa kuwa Sura ya Sita inafaa kupuuzwa ili kuruhusu Uhuru Kenyatta na William Ruto kuwania urais licha ya mashtaka ya uhalifu wa kivita yaliyowakabili katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC), EACC haingefanya lolote.

Tangu wakati huo, imekuwa kawaida kwamba watu wanaochunguzwa au wanaokabiliwa na mashtaka ya jinai wanaweza kuwania nyadhifa za kisiasa bila vizuizi vyovyote.

Wanaweza pia kuteuliwa katika Baraza la Mawaziri, Idara ya Mahakama, Tume za Kikatiba, Vyombo vya Kisheria, Mashirika ya Serikali na afisi nyingine za umma licha ya rekodi zao chafu kimaadili.

Serikali ya Kenya Kwanza haiwezi kuruhusu kupitishwa kwa sheria itakayoondoa pengine robo tatu za baraza la mawaziri la sasa au washikilizi wengine wa afisi kuu za umma.

Neno 'Maadili' ni chafu na la kutisha kwa utawala wa sasa, ambao ni uzao wa utawala



**Serikali ya Kenya Kwanza haiwezi kuruhusu kupitishwa kwa sheria itakayoondoa pengine robo tatu za baraza la mawaziri la sasa au washikilizi wengine wa afisi kuu za umma. Neno 'Maadili' ni chafu na la kutisha kwa utawala wa sasa, ambao ni uzao wa utawala uliopita wa Jubilee, ambao ulikuwa mrithi wa utawala wa Kanu, ulioichukulia serikali kuwa mtambo wa kupora.**

uliopita wa Jubilee, ambao ulikuwa mrithi wa utawala wa Kanu, ulioichukulia serikali kuwa mtambo wa kupora.

Tume ya EACC ilijaribu kutekeleza Sheria ya Maadili wakati wa kuidhinisha wagombeaji katika Uchaguzi Mkuu wa 2022 lakini ikafeli vibaya. Ilibaki kimya serikali ya Ruto ilipopendekeza uteuzi wa watu wanaokabiliwa na masuala ya kimaadili kuhudumu katika nyadhifa za umma. Haikupinga wala kulalamikia hatua hiyo hata kidogo.

Kwa hivyo, sio tu kwamba mapendekezo hayo yamepitwa na wakati, lakini pia ni kazi bure kwa sababu bunge linalodhibitiwa na Kenya Kwanza litayatupa nje haraka.

Hata hayatapita kamati ya idara husika na hayatawahi kuwasilishwa rasmi katika Bunge ili kujadiliwa na kuamuliwa. Iwapo kwa bahati, yatapita kwa kamati, marekebisho ya mwisho yatakuwa hayana uzito, hivyo yatakosa maana yoyote katika utekelezaji wake.

Hilo, hata hivyo, halimaanishi yanafaa kuondolewa. Hata kama inajua kuna uwezekano mdogo wa kupita, EACC inaweza kutumia njia zingine badala ya Bunge. Inaweza kutangaza mapendekezo hayo na kuvumisha mjadala huo kupitia mikutano ya umma nje ya Bunge.

Wananchi wakijitokeza sauti na nguvu kuunga mkono hatua ya kuzuia wezi na watu wahalifu wengine kupata nafasi zaidi kupora mali ya umma, serikali ya Kenya Kwanza italazimika kuzingatia matakwa yao.

Kinachohitajika ni kuuliza ni nani anayekabiliana na ufisadi, na ni nani anayepinga vita dhidi ya ufisadi

Huu unaweza kuwa wakati bora wa kulazimisha viongozi wa serikali na wabunge kuonyesha kama wamejitolea kutetea uadilifu, uwajibikaji na maadili katika uongozi, au uporaji usiodhibitiwa, uharibifu wa taasisi za umma, uhujumu wa uchumi na kufilisisha raia.

Kama Twalib Mbarak na watu wake wamejitolea, watasukuma mapendekezo hayo bila woga katika juhudi za kukabiliana na ufisadi wa kitaasisi. Hata kama watashindwa, watakuwa wameonyesha nia yao, kuanzisha mjadala wa umma na kuwaanika hadharani watetezi na waendeshaji wa ufisadi.

***gaithomail@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Kamau Wanderi*

Nation Media Group

SIASA ZA URITHI

# SIO MJINGA, SI MARA NYINGINE

**Kalonzo Musyoka ameamua kugombea urais 2027 baada ya kumuunga mkono Raila katika chaguzi kuu tatu zilizopita**

● NA OSCAR OBONYO

Wadhifa wa Makamu - (au naibu) Rais, wanasema, ni hatua chache tu kutoka kwa Urais. Stephen Kalonzo Musyoka anajutia siku ambayo aliyekuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma Francis Kimemia na Nick Wanjohi, aliyekuwa katibu wa kibinafsi na mshauri wa aliyekuwa Rais Mwai Kibaki, walidaiwa kuvuruga nafasi yake ya kuwa rais.

Na huku Musyoka akiapa kupigania nafasi aliyopoteza, kupanda kwa Rais William Ruto, aliyeingia mamlakani miezi minne iliyopita kutoka nafasi ya Naibu, Rais ni ukumbusho mchungu wa wa makosa au bahati mbaya ya kisiasa ya kiongozi huyo wa Wiper.


Kwa njia moja, Ruto alitimiza ndoto yake kupitia kampeni za mapema kote nchini kinyume na matakwa ya bosi wake, Uhuru Kenyatta. Si ajabu basi, kuwa Musyoka, aliyeungama kuvutiwa na mbinu ya kampeni ya Ruto, anataka kuanza mapema.

Washirika wake, akiwemo kiongozi wa wachache katika Seneti Enoch Wambua, wanasisitiza kuwa ili Azimio la Umoja One Kenya uweze kushinda uchaguzi mkuu wa 2027, "ni lazima tufanye alichofanya Ruto. Ni lazima tuanze kampeni zetu mapema".

Akihojiwa majuzi na Zainab Ismail katika NTV, Musyoka alisema yeye si mjinga tena, akizungumzia hatua ya kuunga mkono azma ya urais ya Raila Odinga katika chaguzi kuu za 2013, 2017 na 2022. "Mimi si mjinga tena" ni sawa na kujitenga na ushirika wa kisiasa wa Odinga au kumtaka kiongozi wa Orange Democratic Movement (ODM) kuunga azma ya urais ya Kalonzo 2027.

Katika mkutadha huo, kuwa mwerevu kisiasa kunamaanisha kurekebisha makosa ya awali na kunyakua nafasi, kama aliyokabidhiwa Musyoka alipokuwa Makamu Rais. Akikumbuka njama ya urithi wa Kibaki, Musyoka alisimulia katika mahojiano ya kipekee jinsi watu wenye ushawishi katika Ikulu walimdhulumu na kumtupa nje ya uwaniaji urais.

Msaidizi mkuu wa Kibaki katika serikali ya muungano anatoa mfano wa tukio moja mjini Machakos mnamo 2012, Rais alipomuidhinisha hadharani kuwa aliyempendelea kumrithi.




Aliyekuwa Msemaji wa Serikali wakati huo (sasa ni Waziri wa Mashauri ya Kigeni) Dkt Alfred Mutua, hata alituma taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu tukio hilo.

Hata hivyo, msafara wa Rais ulipofika Kitui ambako Kibaki alikuwa mgeni wa heshima katika siku ya upanzi wa miti, taarifa nyingine ilikuwa imetumwa kubadilisha iliyotumwa na Mutua kwa vyombo vya habari.

Kalonzo anahusisha hatua hii na njama za baadhi ya wanasiasa wa eneo la Mlima Kenya, waliomtaka aliyekuwa Mkuu wa Huduma ya Habari za Rais, Isaiah Kabira, kukanusha taarifa ya Mutua. Makamu Rais wa zamani anasema hata alibaini wazi hakuwa akitakiwa aliyekuwa Naibu Waziri Mkuu Musalia Mudavadi alipoingizwa katika mpango wa urithi.

Anadai Wanjohi na Kimemia, ambaye alikuwa gavana wa Nyandarua, waliibuka na chama cha United Democratic Forum ambacho Mudavadi, sasa Mkuu wa Mawaziri katika serikali ya Ruto, alitumia kugombea urais 2013.

Ingawa anadai amepata funzo, ukiwemo ukweli kuwa katika siasa "huwezi kutarajia kitu kwa kupewa", Musyoka anakabiliwa na vizingiti vingi katika azma yake ya hivi punde kuwa rais. Ikizingatiwa Ruto kuwa amepata nguvu kisiasa, kwa kutangazwa mshindi katika uchaguzi wa urais wa Agosti mwaka jana akikumbwa na changamoto nyingi, kitakuwa kibarua kigumu kwa Musyoka kumshinda Rais - ambaye kwa sasa anafurahia ushawishi na kuwa mamlakani - bila usaidizi wa wenzake katika Azimio.

Ingawa ni kweli kuwa Musyoka kufikia sasa amejitoa mhanga kisiasa kumuunga mkono Odinga na anafaa kuungwa mkono na waziri mkuu huyo wa zamani wakati huu, kuna tofauti kati ya viongozi hao wawili na washirika wao kuhusu njia bora ya kushughulikia kampeni za 2027.

Huku washirika wa Musyoka wakitaka atangazwe mgombeaji wa Azimio ili aweze kuanza kampeni mapema, washirika wa Odinga wanamtaka kwanza aunganishe Azimio kwa lengo la kukabili sera za Ruto zisizo maarufu kabla ya kumkabidhi uongozi mtu mwingine.

Akitambua wajibu wa Musyoka

kurunzi ya kenya



Kiongozi wa Muungano wa Azimio la Umoja–One Kenya Raila Odinga, kiongozi wa Wiper Kalonzo Musyoka na kiongozi wa Narc-K Martha Karua wakiwa katika uwanja wa Kamukunji jijini Nairobi mnamo Desemba 7. PICHA IDENNIS ONSONGO

katika maisha ya kisiasa ya Raila, Katibu Mkuu wa Azimio Junet Muhamed anashikilia kuwa nguvu na umoja wa chama hicho cha upinzani katika kutekeleza jukumu lake la kukosoa serikali na kuzuia maovu ya serikali ya Ruto ni muhimu zaidi. Junet, ambaye pia ni Kiranja wa Wachache katika Bunge la Kitaifa, anaomba subira katika kutambua atakayeshindana na Ruto 2027.

Hata hivyo, Makamu Mwenyekiti wa Wiper, Mutula Kilonzo Jr, anasema kiongozi wa chama chake hafai kusubiri kuidhinishwa na Odinga, bali anafaa kuanza kuchukua mwelekeo wa kisiasa kivyake. Akisema ndoto ya Azimio iliisha baada ya kushindwa katika uchaguzi, Gavana huyo wa Makueni anasema wadau wa muungano huo "wako pamoja kugawana vinono vinavyowajia huku wakijiandaa kwa 2027".

Hali ya kutoelewana katika mkakati wa kampeni wa Azimio, ambako kwa upande mmoja kunatokana na matukio ya siku zilizopita kati ya Odinga na Musyoka, ni chanzo cha wasiwasi kwa wanaojua kinachoendelea. Inasemekana Odinga anataka kutekeleza jukumu muhimu katika siasa za upinzani, akiamini kuwa, kama serikali haitafuatiliwa kwa karibu, ufanisi wa demokrasia uliofikiwa kwa miaka mingi unaweza kuharibiwa na serikali ya Ruto.

Kando na Bw Odinga, ni lazima Musyoka amshinde kiongozi wa Narc Kenya, Martha Karua, kupata tikiti ya Azimio, ingawa wengine wanaweza kujitokeza pia. Kwa sasa, Karua anachukuliwa kuwa mkubwa zaidi kuliko kiongozi huyo wa Wiper kutokana na ukweli kuwa alikuwa Mgombea Mwenza wa Urais wa Azimio. Hata hivyo, Musyoka anajivunia ufuasi mkubwa wa kisiasa, kutokana na idadi ya wabunge wa chama chake bungeni.

Lakini pia kuna suala la ufadhili wa kampeni, ambao unaweza kuwa kizingiti kwa azma yake ya urais. Tofauti na Ruto, anaye taka kuiga, Musyoka, amekuwa nje ya serikali kwa miaka kumi iliyopita, kumaanisha kupungua kwa mapato na ushawishi wake. Juhudi zake za kushinikiza Mike Mbuvi Sonko kugombea ugavana Kaunti ya Mombasa kwa tikiti ya chama cha Wiper, zilionekana na wachanganuzi kuwa mkakati na zilizonuiwa kupiga jeki azma yake ya urais 2027.

Mwanasiasa huyo tajiri, aliyehudumu kwa kipindi kifupi kama Gavana wa Nairobi baada ya uchaguzi mkuu wa 2017, amehamia kambi ya Rais Ruto. Musyoka, ambaye hajagombea tena urais tangu mara ya kwanza 2007, hana wafadhili wazito wa uchaguzi wanaofahamika.

Kando na kugombea na kushindwa 2007 kupitia ODM- Kenya, Musyoka amejiunga mara mbili na Raila akiwa mgombea mwenza wake - chini ya Muungano wa Mageuzi na Demokrasia na National Super Alliance, na pia katika Azimio mwaka jana, ambapo alikuwa ametengewa wadhifa wa Waziri Mkuu.

Musyoka pia amehusika na mirengo ya kisiasa kama Kalenjin-Kikuyu-Kamba pamoja na Ruto na Uhuru Kenyatta kabla ya uchaguzi mkuu wa 2013, na One Kenya Alliance uliojumuisha Mudavadi, Spika wa Bunge la Taifa Moses Wetangula na Mwenyekiti wa Kanu Gideon Moi, ambayo ilififia kabla ya uchaguzi.

Hata hivyo, wakati huu, Musyoka, ambaye atatimiza umri wa miaka 70 baadaye mwaka huu, anakabiliwa na mojawapo ya changamoto kuu zaidi tangu alipojiunga na siasa za uchaguzi mnamo 1983. Tangu kifo cha mbabe wa siasa za Ukambani, Mulu Mutisya, 2004, Musyoka amekuwa msemaji wa kisiasa wa eneo hilo - wajibu ambao amekuwa akitekeleza bila upinzani mkali.

Lakini tangu mwaka jana, alipohusika katika vita vikali vya ubabe na waliokuwa magavana wa Machakos, Kitui na Makueni - Mutua, Charity Ngilu na Kivutha Kibwana mtawalia – ngome yake ya Ukambani haijatulia. Kuondoka kwa Mutua kujiunga na Ruto na kuteuliwa Waziri kunafanya uchaguzi wa 2027 kuwa mgumu.

Kitaifa, Musyoka, ndiye mwanasiasa mwenye uzoefu mwingi aliye na azma ya urais. Hajawa na bahati kama Ruto, kwa mfano, aliyeingia Bunge 1997 na kuwa Kiongozi wa Nchi robo karne baadaye, au kama Rigathi Gachagua, aliyepanda cheo kuwa Naibu Rais baada ya muhula mmoja bungeni.

Huku wafuasi wake kitaifa na katika ngome yake ya Ukambani wakiendelea kukosa subira, ni suala la kufa na kupona kwa Musyoka. Kwa mfano, akikosa kumshinda urais 2027, atakuwa na miaka 79 uchaguzi mwingine utakapofanywa 2032. Huu ndio ukweli ambao wafuasi wake, ambao wamekuwa wakimlaumu Odinga kwa sababu ya umri wake, hawangetaka kukabiliana nao.

Wambua, ambaye ni Seneta wa Kitui, anachukulia kiongozi wa chama chake kuwa bora zaidi nchini, kutokana na tajiriba yake pana kama kiongozi wa kisiasa na mpenda amani: "Ni kiongozi ambaye ameunda mtandao mkubwa kwa miaka mingi na viongozi wa nchi kote duniani ambaye atafaidi nchi hii."

Maelezo haya kumhusu Musyoka yanaweza kuwa ya kweli, isipokuwa si rahisi kutimiza ndoto yake ya kisiasa peke yake. Atahitaji kuungwa mkono na vinara wenza wa Azimio - Odinga, Karua na Rais mstaafu Uhuru Kenyatta - miongoni mwa wengine kupata kura, na pesa, kukabiliana na uwezo mkubwa wa kisiasa wa Ruto.

Kwa miongo minne iliyopita ambayo amekuwa katika siasa, Bw Musyoka ameonyesha kuwa mtu mwaminifu, asiye na msimamo mkali, sifa ambazo zinaweza kumfaa kwa mipango yake atakapoita mkutano wa Baraza Kuu la Kitaifa la Chama cha Wiper mwezi ujao.

Mkutano huo, unaonuiwa kuchanganua matukio ya 2022 na kubuni mpango wa kufuata, utatoa ishara za wazi sio tu kuhusu msimamo wa kisiasa wa Musyoka lakini pia hatima ya muungano mkubwa wa upinzani, Azimio.

**oscar.tko@gmail.com**

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group ©

## SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# Sony yazindua kidhibiti kipya kuchezea PS5




Sony imeungana na wataalamu wa ufikivu kutangaza kidhibiti cha PlayStation 5
kwa wachezaji walemavu. Mradi wa Leonardo ni "seti inayoweza kubinafsishwa sana"; ya vitufe, vichochezi na vijiti tofauti ambavyo huruhusu wachezaji kuunda mpangilio unaotosheleza mahitaji yao.

Kidhibiti cha Adaptive cha kampuni ya Microsoft kilichotolewa mnamo 2018, kinauzwa kwa Sh11, 248 katika duka la kampuni hiyo nchini Uingereza - ingawa vifungo vya ziada na vijiti vya furaha vinaweza kugharimu pesa zaidi.

Lakini kwa sasa hakuna tarehe ya kutolewa au bei ya Mradi wa Leonardo. Afisa wa masuala ya burudani wa kampuni ya Sony aliambia BBC kuwa kampuni yake "itafanya juu chini" kusaidia wachezaji kucheza kwa urahisi zaidi, kwa raha zaidi na kwa muda mrefu".

"Tunahisi upana wa chaguzi za ubinafsishaji katika Mradi Leonardo ni wa kipekee ukilinganishwa na vidhibiti vilivyo katika soko leo," akasema.

"Mradi Leonardo unaonyesha hali ya kujitolea kwa kundi letu. Tumetumia miaka 28 ya utaalamu wa kubuni katika PlayStation ili kuunda vifaa vya kudhibiti ambavyo tunatumai vitawafaa wachezaji wengi walemavu."

Mashirika kadhaa ya kutoa misaada yalisaidia, likiwemo AbleGamers la Amerika na SpecialEffect lenye makao yake Uingereza.

Mwanzilishi na afisa mkuu mtendaji wa SpecialEffect, Mick Donegan, alisema "amefurahi sana kuona athari za kidhibiti katika kusaidia kuwezesha mchezo kuwafikia watu wengi zaidi."

Shirika hilo awali lilipigia debe meshadidia kidhibiti cha Adaptive cha kampuni ya Microsoft, ambacho kinafanya kazi rasmi na kompyuta aina ya PC au Xbox pekee.

Watengenezaji wengine, kama vile Hori, pia wametengeneza vidhibiti vinavyoweza kupatikana katika soko.

*- Zimetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# SIMU AINA YA ANDROID SASA KUTUMIA SETILAITI




**Mtandao wa Setilaiti una kasi na ni wa kutegemewa lakini ni ghali kuliko unaotumia kebo ama faiba.**

• LONDON

Ushirika mpya kati ya kampuni ya simu za setilaiti Iridium na kampuni kubwa ya kutengeneza chipu ya Qualcomm utawezesha simu mahsusi za Android kutumia setilaiti baadaye mwaka huu.

Ina maana kuwa mahali ambako hakuna mtandao wa simu za rununu, simu zinaweza kuunganishwa na satelaiti zinazopita ili kutuma na kupokea jumbe.

Chipu za Qualcomm zinapatikana katika simu nyingi za kiwango cha juu zinazotumia Android. Apple ilitangaza sifa ya kuwepo kwa setilaiti katika iPhone 14 Septemba 2022.

Huduma hiyo kwa sasa inapatikana tu kwa kutuma na kupokea jumbe za maandishi wakati wa dharura.

Kampuni ya kutengeneza simu ya Bullit kutoka Uingereza ilikuwa ya kwanza kuzindua huduma yake ya setilaiti, na kuishinda Apple. Yake pia ni kwa matumizi ya dharura na itapatikana katika maeneo maalumu pekee itakapotolewa mara ya kwanza.

Ushirikiano huo mpya utafanya huduma hiyo hiyo kupatikana kwa zaidi ya mamilioni ya watumiaji wa simu, bila kuwaunganisha na bidhaa fulani – lakini ni mtengenezaji tu ambaye ataiwezesha.

Iridium ndio mfumo asili wa simu za setilaiti, uliotuma setilaiti yake ya kwanza kuzunguka 1997. Ilikamilisha uboreshaji wa mtandao wake wa vyombo vya anga 75 mnamo 2019.

Setilaiti hizo hufunika dunia nzima na kuruka katika obiti ya chini, karibu kilomita 780 juu ya Dunia, na vikundi vyao vinaweza kuwasiliana na kila mmoja, kupitisha data kati yao.

Qualcomm ilisema kuwa muundo mpya, unaoitwa Snapdragon Satellite, utaingizwa tu kwenye chipu zake za hali ya juu, kwa hivyo hakuna uwezekano wa kuonekana kwenye vifaa vya hali duni.

Lakini hatimaye itasambazwa kwa tabuleti, vipakatalishi na hata magari, na pia kuwa huduma ambayo haijazuiliwa kwa mawasiliano ya dharura – ingawa kuna uwezekano wa kutozwa malipo.

Kuunganishwa kwa setilaiti kunaaminika kuwa tegemeo kubwa la simu za rununu siku za usoni kwa sababu kutamaliza shida ya sehemu ambazo haziko katika mtandao. Hali hiyo hasa hupatikana sehemu za mashambani au maeneo yaliyo mbali na miji.

Mfumo huo umetumiwa kutoa huduma za mtandao na kampuni kama vile Starlink ya Elon Musk. Mtandao wa setilaiti unafanya kazi kwa kasi na unaweza kutegemewa lakini ni ghali kuliko unaotumia kebo au faiba.

Utumiaji wa setilaiti utategemea sheria za serikali za nchi husika kwa sababu baadhi ya nchi, zikiwemo India na China zimepiga marufuku simu zinazotumia setilaiti.

*- Imetafsiriwa na Kamau Wanderi*

Nation Media Group©

# kurunzi ya afrika

■ VISA VYA MAUAJI NA UTEKAJI NYARA VIMELAZIMU WATU WENGI KUKIMBIA VIJIJI

# MZOZO WA BIAFRA



Kanali Odumegwu Emeka Ojukwu (kushoto) akitangaza uhuru wa Biafra mnamo Mei 30, 1967. Watu wa kabila la Igbo wanaoishi kusini-mashariki mwa Nigeria walijitenga na kutangaza Jamhuri Huru ya Biafra, hatua iliyosababisha vita vikali vya wenyewe kwa wenyewe nchini Nigeria ambapo watu karibu milioni moja waliuawa.

## Kundi la watu wenye silaha linapigania uhuru wa eneo hilo lakini imekuwa vigumu kutofautisha kati ya juhudi zake vitendo vya uhalifu

• LAGOS

Msururu wa mauaji ya kinyama, utekaji nyara na uporaji mali vimewatia hofu wakazi wa kusini-mashariki mwa Nigeria. Kundi la watu wenye silaha linapigania uhuru wa eneo hilo lakini imekuwa vigumu kutofautisha kati ya juhudi zake na vitendo vya uhalifu.

Mapigano hayo yamelazimisha watu kutoroka vijiji walikoishi kwa amani hadi miaka michache iliyopita. "Mjomba wangu alitoroka kwa sababu watu hao walitaka awape pesa za kununua bunduki na risasi. Vijiji vyetu havina watu kwa sababu hao sasa ndio sheria," akasema mwanamume ambaye tutamuita Chike Anyikwa, kumkinga na kundi hilo.

Kwenye kambi zao katika misitu iliyo karibu wapiganaji hao wameunda serikali sambamba kijijini alikozaliwa Anyikwa, na vinginevingi katika jimbo la Imo, ambalo, pamoja na Anambra, yameathirika zaidi na mapigano.

Kambi zingine zinapatikana katika majimbo mengine matatu; Abia, Ebonyi na Enugu, kusini-mashariki - ambayo wapiganaji hao wanataka jimbo huru la Biafra.

Wamenyakua mamlaka ya maafisa wa serikali na watawala wa kitamaduni. Mtu yeyote anayetaka kuandaa sherehe ya ndoa au mazishi ni lazima apate idhini yao - na lazima alipe ada fulani ili apewe kibali.

Viongozi wa kundi hilo pia wamejitwika wajibu wa kusuluhisha mizozo miongoni mwa wanakijiji kuhusu masuala kama haki ya umiliki wa ardhi – ishara udhibiti wao.

Anyikwa anaishi jijini Enugu na - sawa na maelfu ya wengine - hangesherehekea Krismasi mbili zilizopita kijiji mwake, hivyo kukiuka kawaida yake ya kila mwaka kujumuika na jamaa na marafiki kijijini. "Jamaa yangu alifanya ndoa ya kitamaduni kijijini. Hakuna aliyeenda. Kila mtu aliogopa kwenda. Maafisa wa usalama hutoka jiji la Owerri (jiji kuu la

Endelea Uk 26

Kutoka Uk 25

wa usalama hutoka jiji la Owerri (jiji kuu la Imo) kisha hurudi kwa sababu vituo vingi vya polisi vimeharibiwa. "Sheria wanayojua watu ni ya wapiganaji wasiojulikana, wanaosema wanatetea Biafra, lakini tunajua si kweli," akaongeza.

Kuundwa kwa Biafra ni ndoto ya muda mrefu ya watu wengi wa kabila la Igbo wanaotaka kusini-mashariki na sehemu ya Niger Delta kuwa taifa lao huru.

Kutokana naujuzi wa kibiashara, Igbo ni kabila la tatu kwa ukubwa Nigeria, likiwa asilimia 15 ya jumla ya watu 217 milioni nchini humo, kulingana na tovuti ya statista.com.

Kampeni ya kujitenga ilishika kasi miaka ya 1960, afisa wa kijeshi kutoka kabila la Igbo, Emeka Odumegwu Ojukwu, alipotangaza kubuniwa kwa Biafra kufuatia mauaji wa watu kutoka kusini-mashariki wanaoishi kaskazini mwa Nigeria, lakini jaribio la kujitenga lilizimwa baada ya vita vikali vya miaka mitatu vilivyosbabisha vifo vya mamilioni ya watu, njaa na ukosefu wa huduma za matibabu.

Licha ya kufeli kwa kampeni ya Luteni Kanali Ojukwu, suala la kujitenga limekuwepo tangu wakati huo, kwa sasa likiendeshwa kundi la 'Indigenous People of Biafra' (Ipob).

Kundi hilo lilibuniwa 2012 Waigbo wawili wanaoishi Uingereza, Nnamdi Kanu na Uche Mefor, kama vuguvugu la amani, lilianzisha tawi lake la kivita, Eastern Security Network (ESN), kusini-mashariki mwa Nigeria mnamo 2020, likisema lilifanya hivyo kulinda watu Waigbo, ingawa wakosoaji wake wanasema limeazisha mapigano yaliyoleta mahangaiko makubwa.

Serikali ya Nigeria imepiga marufuku Ipob na mahakama moja imelitaja kuwa shirika la "kigaidi". Wakosoaji wa serikali wanasema jaribio la kuvunja kundi hilo kwa kutumia jeshi limeongezea mateso ya raia wanaovamiwa kila mara na wanajeshi vijijini. Vijana hukamatwa na kuzuiliwa au kuuawa kwa kushukiwa kuwa washirika wa kundi hilo.

Hatua ya vikosi vya usalama vya Nigeria kuendelea kumzuilia Kanu, licha ya mahakama kuamuru aachiliwe baada ya kuamua kuwa alikamatwa kinyume cha sheria akiwa ng'ambo, imeonyesha kundi la Ipob haliendeshi shughuli zake kwa umoja. Badala yake limejigawa kwa makundi madogo hasimu, baadhi yakiwa wakorofi zaidi na yasiyo na nidhamu.

# Wapiganaji wana serikali sambamba

Mashambulio katika eneo hilo, ambayo vikosi vya usalama vya Nigeria vinahusisha na kundi hilo, yamesababisha kuuawa kwa mamia ya raia na maafisa wa usalama tangu mapigano yalipoanza 2020.

Wanawake, watoto na wazee hawajasazwa. Katika kisa na kutisha msimu wa Krismasi, video ya mwanamke aliye uchi, na kufungwa mikono, ilisambazwa mitandaoni. Baadaye alitambuliwa kuwa afisa wa jeshi la Nigeria, aliyetembelea nyanya yake jimbo la Abia, wapiganaji walipomteka na wakatoa video ikionyesha wakitisha kumuua.

Mwanajeshi mwingine wa kike aliyekuwa safarini kuhudhuria ndoa yake ya kitamaduni pia alitekwa nyara mnamo Mei 2022. Watekaji walitoa video ikionyesha wakimuua kisha kukatakata mwili wake.

Mpenzi wake, mwanajeshi mstaafu, na binamu yake, pia waliuawa na watu waliodai kuwa wapiganiaji uhuru wa Biafra. Waliomteka walijitambulisha kama Watu Wenye silaha Wasiojulakana. Hivi ndivyo magenge mengi hujitambulisha katika video zao, wakionekana kutania wanahabari ambao mara nyingi huhusisha mapigano katika eneo na wapiganaji wasiojulikana.

Mashahidi waliambia BBC wanajeshi wanachoma makao na biashara vijijini wakitafuta afisa huyo na watekaji wake. Lakini msemaji wa jeshi eneo la Obinze jimbo la Imo, Kapteni Joseph Akubo, alisema jeshi halikuhusika.

Hata hivyo, visa vya aina hiyo ni vya kawaida katika eneo hilo. Katika kisa cha kutisha zaidi, Oktoba 2021, wanajeshi walilaumiwa na wakazi kwa kuchoma zaidi ya nyumba 40 katika kijiji cha Izombe, jimbo la Imo, baada ya wanajeshi wawili na raia mmoja kuuawa katika mapigano kati ya vijana na wanajeshi.

Makundi ya kulinda usalama, yaliyobuniwa kupitia usaidizi wa serikali kusaidia kukabiliana na ukosefu wa usalama, pia yamelaumiwa kwa maovu – kikiwemo kisa cha mauaji ya vijana watano wakitoka kwa harusi katika kijiji cha Awomama, pia jimbo la Imo, Julai 2022.

Chigozie Ekesinachi, ambaye ndugu zake wawili ni miongoni mwa waliouawa, alisema mauaji hayo yalitekelezwa na kundi la usalama la Ebubeagu linaloungwa mkono na serikali. Aliongeza kuwa walinda usalama hao walimpiga pamoja na jamaa zake na kuwazuilia walipojitambulisha kuwa jamaa wa watu walioeuawa, ambao miili yao bado ilikuwa katika eneo la mauaji hayo. Baadaye, Idara ya Usalama wa Kitaifa (DSS) ilikubali kuhusika na mauaji hayo, ikisema watu hao walikuwa wapiganaji wa kundi la wanaotaka kujitenga.

Watu waliojitambulisha kuwa wanachama wa kundi hilo pia wamelaumiwa kwa kulenga raia - mnamo Desemba 2022, viongozi wawili wa kitamaduni pia walitekwa kutoka makwao. Mmoja wao, Paul Ogbu, aliuawa na mwili wake ukatupwa ndani ya shimo pamoja na miili mingine iliyooza, huku vikosi vya usalama vikiokoa kiongozi mwingine wa kitamaduni, Acho Ndukwe, kutoka kambi ya wapiganaji hao. Video iliyotolewa baadaye ilionyesha wazee wawili wakiteswa na kulaumiwa kwa kupinga kampeni za uhuru wa Biafra.

Viongozi wengine kadhaa wa kitamaduni pia wamewahi kutekwa, makao yao kuchomwa au kuuawa na watu wanaotaka kujitenga.

Chidiebube Okeoma, mwanahabari wa gazeti la Punch jimbo la Imo, alisema ukosefu wa usalama umeingia mji mkuu wa jimbo hilo. "Owerri ilikuwa maarufu kwa shughuli zake za usiku, lakini hayo sasa hayapo kutokana na visa vya mauaji. Watu kiona sura ngeni wanajificha. Gurudumu la gari likipasuka, watu wanakimbia. Imo haikuwa hivi," akasema.

Jiji hilo, sawa na mingine kusini-mashariki huwa halina watu kila Jumatatu, kutokana amri ya wapiganaji ya "kutotoka nje". Hali hiyo imefanya wanafunzi kukosa mitihani na biashara kupata hasara kubwa. "Hata magavana wote wako ndani ya nyumba zao za serikali, kutii amri ya kutotoka nje," anasema Anyikwa.

Anahofia watu wengi eneo la kusini-mashariki hawataweza kupiga kura katika uchaguzi mkuu mwezi ujao kwa sababu baadhi ya wapiganaji wamewataka wasusie.

Isitoshe, watu wenye silaha, wanaodai kutetea uhuru wa Biafra, wameshambulia afisi za Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC) na watu wanaosajiliwa kupiga kura. Pia waliua mfanyakazi wa INEC 2022.

"Naona aibu kuhusu ukosefu wa usalama kusini-mashariki," akasema Anyikwa. Kwa sasa, mapigano haya hayaonekani kumalizika.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Askari wawili watoto wa jeshi la Biafra wakiwa katika eneo la Umuahia huku jeshi la serikali ya Nigeria likivamia wakati wa vita vya Biafra mnamo Agosti 31, 1968.

# kurunzi ya dunia

■ MAMBO 11 MIHIMU KUTOKA KWA WASIFU WA PRINCE HARRY

# MASAIBU YA MWANAMFALME



Prince Harry (kushoto) na Prince William wakihudhuria hafla ya kuzinduliwa kwa sanamu ya mama yao, Princess Diana katika bustani ya The Sunken Garden Ikulu ya Kensington, jijini London, mnamo Julai 1, 2021. Prince Harry anasimulia katika kitabu chake kipya jinsi "alishambuliwa" na kaka yake mkubwa walipogombana mnamo 2019.

## Kitabu hicho kinafichua machache kutokana na habari zilizovuja na mahojiano na watu maarufu lakini kinaelezea matukio kwa upana

• NEW YORK

"Spare", kitabu cha wasifu kinachongojewa kwa hamu cha Prince Harry, kimevutia watu kote duniani, na kuna ishara kitakuwa kimoja cha vitabu maarufu mwaka huu.

Mahojiano na watu maarufu, na sehemu zilizovuja na kuuzwa kwa kitabu hicho kabla ya kutolewa rasmi Uhispania, kumeongeza hamu ya kitabu kinachoelezea ukweli kuhusu maisha ya Harry.

Harry anasema aliamua kuandika "Spare" alipozuru Uingereza kwa mazishi ya babu yake mnamo Aprili 2021. Hapo alipata ukweli wa "kushangaza" kuwa kati ya baba yake au kaka yake, hakuna aliyeelewa ukweli kuhusu ni kwa nini yeye na mkewe, Meghan, walihamia California. "Lazima niwaambie," aliwaza. "Na hivyo basi: Baba? Willy? Dunia? Karibuni."

### Kifo cha Malika Diana

Asubuhi ya baada ya Diana, mama ya Harry, kufariki katika ajali ya gari jijini Paris, baba yake Charles, alimwamsha kumuarifu kilichokuwa kimetokea. "Aliketi kwenye ukingo wa kitanda," Anaandika Harry. "Aliwekelea mkono kwenye goti langu. Mvulana kipenzi, mama alimehusika katika ajali ya gari," aliendelea. "Walijaribu, mvulana kipenzi. Ninasikikitika hakunusurika."

Harry anaandika kuwa "hakuna chochote nilichomwambia siku hiyo kimebaki katika kumbukumbu zangu. Inawezekana sikusema chochote. Ninachoweza kukumbuka wazi ni kuwa sikulia. "Hata tone la chozi. Baba hakunikumbatia. Hakuwa mzuri wa kuonyesha hisia katika hali za kawaida, angewezaje kutarajiwa kuzionyesha katika shida kama hiyo? Lakini mkono wake haukubanduka mara moja kutoka kwa goti langu na akasema: Itakuwa sawa. Hiyo haikuwa kawaida kwake. Baba, mwenye matumaini, mwenye huruma. Si kweli kabisa."

Miaka mingi baada ya kifo cha mama yake, Harry aliomba aonyeshwe faili za siri za polisi kuhusu ajali hiyo. Karani wa kibinafsi wa Harry alipata faili hizo, ingawa alitoa tu zilizokuwa na "changamoto", Harry aliandika. Na bado, aliona picha nyingi za paparazzi za mama yake aki-

Endelea Uk 28

Nation Media Group ©

kurunzi ya dunia

# Harry na mkewe, Meghan walipohisi kutengwa

Kutoka Uk 27

fariki. Wanaume waliomfuata "hawakuacha kumpiga picha alipokuwa amelala katikati ya viti, akiwa amezirai au kabla ya kuzirai kabisa," anaandika. "Hakuna hata mmoja aliyeangalia hali yake, kumsaidia, hata kumfariji. Walikuwa tu wakipiga picha, kupiga, kupiga, kupiga."

**Walimsihi Charles asimuoe Camilla**

"Tulipoulizwa, mimi na Willy tuliahidi baba kuwa tungemkaribisha Camilla katika familia yetu." Anaandika Harry. "Kitu cha pekee ambacho tulimuomba kilikuwa ni asimuoe. Huhitaji kuoa tena, tulimsihi….. tunakuunga mkono, tunakubali Camilla, tulisema. Lakini tafadhali usimuoe."

**Mambo ya familia kufikia wanahabari**

Kulingana na kitabu hicho, Charles na wakati mwingine Camilla waliidhinisha habari mbaya kuhusu Harry na William kufikia wanahabari. Katika tukio moja, anaandika Harry, Charles - kwa ushauri wa mtaalamu wa porojo - alishirikiana na majarida kuhusu habari za Harry na mihadarati ili kupiga jeki sifa zake zilizokuwa zimeshuka.

"Si mume asiyemwaminifu tena, Baba angekuwa sasa amewasilishwa kwa dunia kama baba asiye na mke, anayeshughulika na mtoto aliyetekwa na dawa za kulevya." Baada ya miaka mingi, mnamo 2019, Harry anaandika kuwa, William alikuwa "akichemka kwa hasira" kwa sababu "Watu wa Baba na Camilla walibuni habari kumhusu, na Kate, na watoto, na hangeendelea kuvumilia. Ukiwapa Baba na Camilla kidogo tu, alisema, wanachukua kila kitu.

Kwingineko, ripoti kuwa Harry na Meghan walikuwa wakihama England zilihusu uvumi ambao Harry anaamini ulitolewa na ikulu ya kifalme. Habari hizo, zilizochapishwa na jarida la The Sun, "zilijumuisha habari za kina kuwa tulikuwa tumeamua kuacha majina ya wanawafalme wa Sussex," anaandika Harry. "Kulikuwa na stakabadhi moja duniani ambapo maelezo hayo yalitajwa - barua yangu ya kibinafsi na ya siri kwa baba yangu. Barua ambayo inashangaza, ni idadi ndogo ya watu waliweza kuipata. Hata hatukuwa tumeitaja kwa marafiki wetu wa karibu."

**Aliua wapiganaji 25 wa Taliban**

"Wanajeshi wengi hawawezi kukueleza ukweli kuhusu idadi ya watu ambao wameua," Harry anaandika kuhusu siku zake katika vita. "Idadi yangu: 25." Anaongeza: "Nilipokuwa katika mapigano, sikufikiri hao 25 walikuwa watu. Huwezi kuua watu ukifikiri kuwahusu. Walikuwa visanamu vya mchezo wa chesi vilivyoondolewa kwenye ubao wa chesi. Wadudu walioondolewa kabla ya kuharibu bidhaa. Nimefunzwa kuwamaliza, nimefunzwa vyema. Katika kiwango fulani, niligundua mafunzo haya yalikuwa shida. Lakini pia niliyaona kama sehemu ya uanajeshi isiyoepukika.



Meghan na Prince Harry katika kongamano la kila mwaka la One Young World Summit katika Ukumbi wa Bridgewater mjini Manchester, mnamo Septemba 5, 2022.

**Alikumbwa na wasiwasi na woga**

Hofu ya kuongea hadharani iligeuka kuwa woga mbele ya umati, kisha wasiwasi mkubwa akielekea kuadhimisha mwaka wa 30 wa kuzaliwa. Katika kitabu hicho, Harry anaona hali hiyo kama aina ya maradhi ya kiakili, akiyahusisha na huduma yake katika jeshi na kifo cha mama yake. Alipomweleza baba yake kilichokuwa kikitendeka, Charles alisema: "Nafikiri ni makosa yangu, ningekupatia usaidizi uliohitaji miaka iliyopita." Anaandika Harry: "Nilimhakikishia hayakuwa makosa yake. Lakini nikakubali radhi yake."

**Kisa kibaya cha ugonjwa wa kuganda**

Ziara moja Eneo la Kaskazini ilimuacha Harry akiugua. "Baada ya kufika nyumbani nilishtuka kugundua sehemu zangu nyeti zilikuwa zimeganda pia, na masikio na mashavu yalipokuwa yakipona, uume wangu haukuwa ukipona," anasema. Matibabu ya nyumbani yalipokosa kumsaidia alimuona daktari.

Jioni moja wakati wa uchumba wao, "Meghan alisema kitu ambacho nilielewa vibaya," kwa hivyo "nilimfokea kwa ukali - kwa ukatili." Meghan aliondoka. "Nilimpata ameketi katika chumba cha kulala. Alikuwa ametulia, lakini akasema kwa sauti ya chini kuwa hangevumilia kufokewa hivyo," anaandika Harry. Alitaka kujua ni kwa nini. *Sijui.*

*Ulisikia wapi mwanamume akizungumzia mwanamke namna hiyo? Uliwasikia watu wazima wakizungumza hivyo ulipokuwa ukikua?*

Nilisafisha koo, nikatazama kando. *Ndio*. Harry alimwambia Meghan alikuwa amejaribu matibabu, lakini hayakumsaidia. "Hapana," alimwambia. "Jaribu tena."

**Hakuna pesa za kumsaidia na Meghan**

Mazungumzo kati ya baba na mwanawe Harry alipotangaza nia yake ya kuoa hayakwenda alivyotarajia.

*Anataka kuendelea kufanya kazi?*
*Unaulizaje?*
*Anataka kuendelea kuigiza?*

*"Oh, sijui, sidhani anataka hivyo. Natarajia atataka kuwa nami, kufanya kazi, wajua, ambayo itamaanisha kutovaa "suti"…. kwa kuwa wanaigizia … Toronto.*

*Hmm, Sawa. Naam, mvulana kipenzi, unajua hakuna pesa za kutosha kutembea kila mahali.* Nilikodoa macho. Alimaanisha nini?

Akaelezea. *Au kujaribu kufanya hivyo. Siwezi kulipia kila mtu. Tayari ninalipia kaka yako na Catherine.*

Anaandika Harry: "Baba hakunisaidia kifedha mimi na Willy, na familia zetu….Tulikubali kuhudumia ufalme, kwenda walikoenda, kufanya tulichoambiwa, kuacha uhuru wetu, kuishi kama wafungwa kila wakati, nao walitufungia walikubali kutulisha na kutuvisha.

Lakini haikuwa kuhusu pesa, bila shaka: Inawezekana Baba aliogopa kuongezeka kwa gharama ya kututunza, lakini kile ambacho hangekubali ni mtu mpya kutambulika katika ufalme, kunyakua umaarufu, mtu anayeng'aa na kumzidi umaarufu."

**William hakutaka Harry kusimamia arusi**

"Umma ulikuwa umefahamishwa nilikuwa msimamizi wa bwana harusi, lakini huo ulikuwa uongo," anaandika. "Willy hakutaka nitoe hotuba ya msimamizi wa bwana harusi. Hakufikiri ilikuwa salama kunipa kipaza sauti nizungumze. Hakukosea." Licha ya hilo, aliwakabidhi wanandoa wapya suruali ya mwanamke katika sherehe ya harusi. "Pumzi ziliwapaa waliokuwa ukumbini," anaandika, "kisha wimbi la kicheko cha furaha."

**Lawama kwa kampuni ya Murdoch**

"Sikudhani kuna binadamu katika historia ya miaka 300,000 ya aina hii ya viumbe alituharibia ukweli wetu wa pamoja," anasema. Lakini walioajiriwa kupiga picha za majarida ya Uingereza wanalengwa na hasira zake pia. "Wapiga picha wamekuwa watu wa kutisha, lakini nilipokomaa, walikuwa wabaya zaidi," anasema. "Walikuwa na ujasiri zaidi, wakali zaidi, jinsi vijana wa Iraq walivyopewa mafunzo makali. Walimu wao ni wahariri, walioahidi kufanya vyema baada ya mama kufariki."

**Harry na Meghan walihisi kutengwa**

Wawili hao walichagua kuondoka Uingereza, lakini walitarajia kudumisha baadhi ya majukumu yao ya kifalme na kudumisha ulinzi unaotokana na hadhi zao. Baada ya mkutano ulioitwa "Kongamano la Sandringham" Januari 2020, walijua, kulingana na Harry, "tumeisha" - hawatawakilisha malkia tena na ulinzi wao ungeendelea kwa miezi 12 ya kipindi cha mpito. "Naipenda nchi yangu ya kuzaliwa, na naipenda familia yangu, na nitaendelea kuipenda," anaandika Harry. "Ninatamani tu, katika tukio la pili baya zaidi katika maisha yangu, wote wawili wangenisaidia."

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Nation Media Group©

kurunzi ya dunia

■ HASIRA YAKE KWA WANAHABARI NI KUBWA

# KITABU CHA AJABU CHA KIFALME

## Kuna maelezo kumhusu kama mvutaji bangi, akivuta baada ya chakula cha jioni na kuhofia moshi utamfikia mzee jirani yake

● LONDON

Kitabu cha wasifu wa Mwanamfalme Harry, 'Spare' ni nusu ungamo, nusu ujumbe wa hasira na nusu barua ya kimapenzi. Sehemu zingine ni kama ujumbe mrefu zaidi kuwahi kutumwa na mlevi.

Kimeandikwa kwa uwazi na mapenzi - kikionyesha uajabu wa maisha yake ambayo mara nyingi ni ya upweke. Na ni maelezo madogo, badala ya makubwa, yanayoonyesha jinsi tunavyojua machache. Kuna maelezo kumhusu kama mvutaji bangi, akivuta bangi baada ya chakula cha jioni na kuhofia moshi utamfikia mzee jirani yake.

Nani mwingine wa familia ya kifalme anayeweza kuelezea jinsi alivyopoteza ubikira wake nyuma ya baa na kuhusu uume wake uliogandishwa na baridi kali? Harry anazungumziwa zaidi kuliko jamaa zake wengine. Labda kunapaswa kuwa na tahadhari kwa mengi yanayofichwa kumhusu. Aidha, alifahamu kuhusu wasichana "wenye kupenda mamlaka" ambao watakuwa "wakivalia taji la mamlaka mara baada ya salamu ya mkono."

Kuna kisa akiwa katika Ikulu ya Buckingham wakati wa tamasha ya ukumbusho na akisikiza Brian May akicheza kwenye paa - na anagundua nyanya yake, Malkia Elizabeth, amevaa vizibo masikioni. Maisha yake jijini London kabla hajamuoa Meghan yalijaa starehe lakini pia anaonekana kama mtu aliyeishi mafichoni.

Harry alikuwa akikumbwa na hali za kutisha za mshtuko, mbaya kwa mtu yeyote, lakini za kudhoofisha kwa mtu anayetarajiwa kuongea na kuonekana hadharani. Anaelezea maisha yake ya upweke nyumbani, akitumia dawa za kupoteza fahamu, akikausha nguo zake kwa stima na kupanga ziara za kwenda kununua bidhaa kama mavamizi ya kijeshi; yanayofanywa kwa njia kisiri na haraka.

Hana akaunti ya duka la Amazon, lakini hufika katika maduka ya TK Maxx kununua nguo, na hununua vyakula kila wiki katika duka moja kubwa akitafuta samaki aina ya 'salmon' na maziwa yaliyoganda.

Siku moja akiwa humo anasikia wanunuzi wakiulizana iwapo yeye ni shoga. Lakini ni maisha yasiyo ya kawaida, ghafla akikosa saa ya kutangamana na marafiki wa kimataifa.

Harry anasema hutazama mchezo wa kuigiza wa runinga unaojulikana kama, 'Friends on a loop', akimpenda mhusika mcheshi Chandler. Lakini akiwa ziarani Amerika anajipata kwenye karamu na Courtney Cox, mwanamke anayeigiza kama Monica, mkewe Chandler katika mchezo huo.




Kazi hiyo aliyoandikiwa inajumuisha mambo mengi, yanayoelezwa haraka na yanaangazia masuala ya ndani, aghalabu akifahamu kuna walinzi nje ya mlango na kamera zinazomsubiri. Kama mwanafunzi wa shule, akivuta bangi na marafiki wake, anatazama polisi hapo nje kumlinda.

Katika hadithi hii, karibu kila ukurasa, kuna hofu kubwa ambayo inaonekana kuvuruga maisha yake yote - kifo cha mama yake Diana.

Alimpenda sana na majonzi kuhusu kifo chake yalizidi aina nyingine za wasiwasi alizokuwa nazo. Anachukia sana wanahabari, akiwalaumu kwa kumfuata mama yake kila mara, ikiwemo wakati wa kifo chake kupitia ajali jijini Paris, huku akirejelea eneo la ajali hiyo. Hasira yake kwa wanahabari ni kubwa, lakini zaidi kwa Rupert Murdoch, huku mmoja wa maafisa wake wakuu akielezewa tu bila kutajwa jina.

Ugomvi kati yake na kaka yake William mara nyingi huelezewa kwa kurejelea ukaribu waliokuwa nao na mama yao.

Wasiwasi wake mkubwa na maisha ya kutojali yanaonekana kuwa matokeo ya kumpoteza mama yake, na kupoteza nguzo kuu ambayo hadi alipokutana na Meghan, hakuwa amepata nyingine.

Pia ana tatizo la kupenda kifo. Akienda katika Westminster Abbey kwa harusi ya kaka yake, kwa furaha anafikiri kuhusu karibu watu 3,000 waliozikwa katika kanisa hilo katika karne kadhaa.

Kinachokosekana katika kitabu hicho ni hali ya kufahamu hali ya ulimwengu mpana nje. Ni kama kwamba amepofushwa na mwangaza wa wapiga picha. Hakuna anayejali kulipa bili za gesi katika kitabu hiki. Anazuru Afrika mara kadhaa kana kwamba ni vituo vichache katika Eneo la Kaskazini. Ingawa hiyo ingekuwa hali ya kisasa kwake kwa sababu anasema wakati alitumia treni aina ya Tube ni alipoenda katika ziara ya kimasomo.

Anaelezea wazi maisha ya ufalme - ndiyo huyo ni baba yake akifanya mazoezi ya viungo akivalia suruali fupi - kitabu hakielezei maoni yoyote kuhusu maisha ya nje, ingawa sasa hatekelezi majukumu ya kifalme.

Harry anaongea kuhusu Mwanamfalme William, akifanya kila anachokitaja "hotuba inayopinga Brexit" inayoonekana kukasirisha magazeti. "Brexit ndiyo ilikuwa riziki yao. Anawezaje kuitaja kuwa upuuzi," anaandika. Watu wengine wa familia ya kifalme wanadaiwa na Harry kujihusisha zaidi na idadi ya ziara ambazo wamefanya wakilinganishwa na watu wengine wa familia hiyo. Wanatazama nyuma kuona kama kuna mtu yeyote anapaswa kuhoji umuhimu wao.

Lakini hata hivyo, yeye pia ni kiumbe wa malezi yake mwenyewe, akielezea kupiga risasi swara kwa namna ya kipekee.

Nani atakasirishwa zaidi na ufichuzi huu wote katika kitabu chake? Zaidi kampuni ya Netflix. Ililipa pesa nyingi kwa mahojiano marefu ya televisheni na maelezo katika mtandao wa Instagram.

Kitabubu hicho na kitu cha ajabu katika karibu kila ukurasa. Sehemu yake kubwa itawafanya watu kukerwa. Anazungumzia kuhusu mzozo wa watu karibu na makao yake na maelezo ya kina kuliko ambayo ungetarajia kutoka kwa vita vidogo.

Pia kuna madai ya kufurahisha kama vile kulinganisha "kampeni kuhusu masuala ya ngono" ya kundi la wasichana la Spice Girls na mapambano ya Mandela dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Sehemu iliyofichuka ya kitabu hicho inajikita katika mizozo ya kifamilia huku Harry akilalamika kuwa hakuna anayemsaidia yeye na Meghan. Camilla anatokea katika hadithi kuwa mama yake wa kambo, huku maelezo kumhusu yakiwa mseto wa tuhuma na juhudi za kuwa mpole.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

# TANZIA

## ALIKUWA MSHAMBULIZI STADI ENZI ZAKE

**Sifa za Mwitaliano huyo zilidhihirika kupitia taaluma ya uchezaji na usimamizi, na pia kutokana na nafsi yake ya kuvutia na kuheshimika iliyomfanya kipenzi cha wengi katika kandanda kote duniani**




Gianluca Vialli kabla ya mechi ya fainli ya Euro 2020 kati ya Italia na Uingereza jijini Wembley mnamo Julai 11, 2021.

Gianluca Vialli alifariki Januari 6, akiwa na umri wa miaka 58.

• ROMA

Gianluca Vialli, aliyeaga dunia Januari 6 akiwa na miaka 58, alikuwa mmoja wa washambulizi nyota wa kizazi kipya na pia maarufu. Sifa ya Mwitaliano huyo ilidhihirika kupitia taaluma ya uchezaji na usimamizi, na pia kutokana na nafsi yake ya kuvutia na kuheshimika iliyomfanya kipenzi cha wengi katika kandanda kote duniani.

Vialli alichezea Italia mara 59 baada ya kucheza kwa mara ya kwanza 1985, akichezea timu ndogo ya Cremonese kabla ya kung'aa zaidi katika timu ya Sampdoria kisha Juventus na Chelsea, ambako alikuwa mchezaji na meneja mashuhuri.

Alikuwa mshambulizi mwenye nguvu na kasi lakini pia aliyeweza kuonyesha ustadi, angani na ardhini huku akiibuka kuwa kigogo wa kupigiwa mfano.

Alikuwa mchezaji wa kutegemewa katika Sampdoria, ambako aliunda ushirikiano hatari wa kushambulia kati yake na Roberto Mancini. Huu ulikuwa urafiki wa muda mrefu uliomwezesha kuwa mmoja wa wasaidizi wa kocha wa timu ya Italia iliposhinda Kombe la Euro 2020 kwa kuishinda Uingereza katika fainali kupitia mikwaju ya penalty katika uwanja wa Wembley.

Akichezea Sampdoria, Vialli alikuwa kiungo muhimu wa timu iliyoshinda Kombe la Washindi Uropa 1990, ambapo alifunga mabao yote mawili muda wa ziada na kushinda 2-0 dhidi ya Anderlecht jijini Gothenburg. Kisha aliongoza Sampdoria iliposhinda taji lake la kwanza la Serie A 1990-91 lakini walivunjika moyo waliposhindwa na Barcelona katika fainali ya 1992 ya Kombe la Uropa jijini Wembley, mechi iliyotamatishwa na mkwaju wa Ronald Koeman muda wa ziada. Wakati huo Sampdoria pia ilishinda kombe la Coppa Italia mara tatu.

Ilikuwa lazima kwa Juventus kumsaka kwani aliwapa mabao 141 katika misimu minane, kisha akaondoka na kujiunga na Turin kwa ada ya kihistoria enzi hizo ya pauni 12 milioni (Sh1.8 bilioni).

Chini ya uongozi wa kocha mashuhuri Marcello Lippi ambaye baadaye alishindia Italia Kombe la Dunia, Vialli alibobea hata zaidi, huku akiimarika kimiondoko na kiufundi, na kuchangia nafasi muhimu katika timu iliyogeuka kuwa moja ya klabu bora zaidi Italia.

Vialli alikuwa katika timu ya Juventus iliyoshinda Kombe la Uefa 1993 kwa jumla ya mabao 6-1 dhidi ya Borussia Dortmund kwa misimu miwili. Alikaribia kushinda msimu wa tatu 1995 lakini Juventus ikashindwa na Parma. Ni msimu huo ambao walishinda tuzo la Serie A na Coppa Italia.

Alikamilisha muda wake Juventus akiwa kileleni kama nahodha alipoongoza timu ya 'The Old Lady' kunyakua ushindi katika fainali za Ligi ya Mabingwa 1996 kwa kuichapa Ajax 4-2 kupitia mikwaju ya penalti jijini Roma.

Vialli kisha alijiunga na Chelsea kwa uhamisho huru katika juhudi za Ruud Gullit kuimarisha timu hiyo. Kwa mara nyingine, Vialli alipata umaarufu mara moja kupitia tabia yake ya upole na nidhamu katika kandanda na maisha licha ya ufanisi na hadhi ambayo talanta yake ilikuwa imemletea.

Vialli hakuvuma sana siku za mwanzoni katika Chelsea, na aliitwa kucheza dakika za mwisho kuchukua nafasi ya Gianfranco Zola waliposhinda Middlesbrough katika fainali ya Kombe la FA mnamo 1997.

Mmiliki wa Chelsea Ken Bates alibahatisha kwa kumteua Vialli, 33, kuwa mchezaji na pia meneja mambo yalipomwendea vibaya Gullit mapema 1998, lakini matokeo yalikuwa mazuri. Katika miezi sita kadhaa alitimiza majukumu yote mawili kwa timu hiyo iliyoshinda Kombe la Washindi Uropa dhidi ya VfB Stuttgart jijini Stockholm kupitia bao la Zola.

Walikuwa tayari wameshinda Kombe la Ligi kwa kulaza Middlesbrough 2-0 jijini Wembley huku Vialli akiingia kipindi ambacho kilimweka katika simulizi za timu ya Chelsea milele. Chelsea ya Vialli pia ilishinda European Super Cup dhidi ya Real Madrid, kabla ya kuacha kucheza na kushughulikia usimamizi.

Vialli alipata ushindi mkubwa wa mwisho Chelsea iliposhinda Aston Villa na kunyakua Kombe la FA jijini Wembley mnamo Mei 2000, lakini akafutwa kazi baada ya matokeo mabaya msimu uliofuata.

Alirudi kama msimamizi wa timu ya reja kwenye Daraja la Kwanza ya Watford hakufaulu na akafutwa baada ya msimu mmoja wa matokeo mabaya katika Vicarage Road.

Hekima na hulka yake ya kutangamana na watu zilimfanya atafutwe na wengi ili kutoa ushauri kuhusu kandanda. Alikuwa mmoja wa maafisa wa Italia wakati wa mashindano ya Euro 2020 akiwa amevalia suti maradidadi huku akitabasamu baada ya ushindi.

Itakumbukwa kama hali ya kuvuta hisia nyota hao wawili Vialli na Mancini, tofauti kitabia lakini wakifanana kwa mambo mengi na kuunganishwa na kandanda na urafiki wa dhati, walipokumbatiana kwa muda mrefu huku wakitiririkwa na machozi ya furaha baada ya ushindi katika uwanja Wembley baada ya ushindi.

– BBC

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

# GET YOUR FAVOURITE DAILIES DELIVERED TO YOUR HOME

Fresh and unbiased news delivered to your doorstep





SMS the word **GAZETI** to **20567**,
Share your preferred delivery location
and our agent will get in touch with you

**FREE** SMS text and **FREE** Delivery

DAILY NATION | Business Daily | TAIFA LEO | The EastAfrican

Terms & Conditions apply*


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM